**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA BAJETI YA WIZIRI WA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO

**MHESHIMIWA DKT. RIZIKI PEMBE JUMA**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/2027**

## YALIYOMO


**A. UTANGULIZI ........................................................................ 1**

**B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.............................. 3**

**C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026............... 4**

C.1. Fedha zilizopatikana kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ............................................................................. 4

C.2Ukusanyaji wa Mapato kwa Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ............................................................................. 5

C.3. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026.............................................................. 5

C.4.1. PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI................................................................ 6

C.4.2 PROGRAMU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO ...........................................................................15

C.4.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA ZA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO....................................29

C.4.4 PROGRAM YA MAENDELEO YA VIJANA.........................................34

C. 5Mafanikio na Changamoto za Wizara kwa Kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026.............................................................35

C.5.1 Mafanikio ...................................................................35

C.5.2 Changamoto.................................................................38

**D. MUELEKEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ...........................................................39**

1.1. IPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ...........................................................40

D.2. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 ...........................................................40

FUNGU O56 WIZARA YA HABARI SANAA UTAMADUNI NA MICHEZO.......................................................................41

D.2.1. PROGRAMU YA MENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI ....41
D.2.2. PROGRAMU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO ....45
D.2.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO....50
FUNGU 107: TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR ....53
D. 3PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI NA UTANGAZAJI ....53
D.3.1 Programu Ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji ....53
D.3.2 Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji ....53
**F: MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/ 2027 ....54**
FUNGU 056....54
FUNGU 107....55
**G. SHUKURANI ....55**
**VIAMBATANISHO ....58**
*KIAMBATISHO NAMBA 1 A* .... 58
*KIAMBATISHO NAMBA 1B*.... 62
MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2024 HADI MACHI 2025 ....62
*KIAMBATISHO NAMBA 1C*.... 62
MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA ....62
*KIAMBATISHO NAMBA 1D*.... 63
FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 KWA KILA PROGRAMU NDOGO ....63
*KIAMBATISHO NAMBA 1E*.... 66
*KIAMBATISHO NAMBA 1F*.... 68
*KIAMBATISHO NAMBA 1G* .... 70
BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027....70
KWA KILA PROGRAMU NDOGO ....70
Tume ya Utangazaji Zanzibar....72
*KIAMBATISHI NAMBA 1H* .... 72
*KIAMBATISHI NAMBA 1I*.... 73
*KIAMBATISHI NAMBA 1J* .... 74

## UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na kupitisha utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 pamoja na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima, afya njema na kutuwezesha kukutana katika kikao hiki muhimu kwa ajili ya kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara na mipango ya maendeleo kwa ustawi wa wananchi wa Zanzibar. Aidha, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuibariki nchi yetu kuendelea kuwa na amani, utulivu na mshikamano unaotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

3. **Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,** kwa kupewa tena imani kwa mara ya pili na wazanzibari katika kuingoza Zanzibar kwa kushinda kwa kishindo katika uchaguzi uliofanyika mwezi Oktoba, 2025. Aidha, kwa mara nyengine tena ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi kwa uongozi wake thabiti, wenye maono na unaolenga maendeleo jumuishi ya wananchi. Dira yake imeendelea kuleta matumaini mapya, kuimarisha ustawi wa jamii pamoja na kukuza uchumi wa Zanzibar kwa kasi na ufanisi mkubwa. Tunamshukuru kwa juhudi zake zisizochoka katika kuleta mageuzi chanya na tunamuombea afya njema na mafanikio zaidi ili aendelee kuiongoza nchi yetu kuelekea ustawi na maendeleo endelevu.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluh Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** kwa kuchaguliwa na wananchi kwa ushindi wa kishindo

kuiongoza Tanzania katika uchaguzi uliofanyika Oktoba 2025, vile vile, ninampongeza kwa moyo wake thabiti wa kuwapenda wananchi wa Tanzania na uongozi bora wa kuleta maendeleo nchini. Tunatambua jitihada zake za kukuza uchumi, kuimarisha huduma za jamii na kuheshimu misingi ya uwazi na uwajibikaji, tunamuombea hekima, afya na mafanikio zaidi katika kuendelea kuhudumia taifa letu.

5. **Mheshimiwa Spika,** vile vile nampongeza **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla,** Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia shughuli za Serikali kwa ufanisi mkubwa pamoja na kuchangia kwa dhati utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025–2030. Uongozi wake umeendelea kuwa chachu ya uwajibikaji, mshikamano na kasi ya maendeleo katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali, jambo linaloleta matumaini makubwa kwa wananchi.
Aidha, napenda kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika pamoja na wenyeviti wa Baraza kwa kuliongoza Baraza hili tukufu kwa umakini na umahiri wa hali ya juu katika kufikia maamuzi mbalimbali yenye manufaa kwa ustawi wa Wazanzibari. Mchango wenu ni muhimu sana katika kuhakikisha kuwa malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa kwa ufanisi na kwa manufaa ya taifa. Mwenyezi Mungu awajaalie afya njema na hekima zaidi ili muendelee kutekeleza wajibu wenu kwa uadilifu na mafanikio makubwa.

6. **Mheshimiwa Spika,** shukrani zangu za dhati kabisa ziende kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi kwa maoni, ushauri na mapendekezo mazuri wanayotupatia kila tunapokutana kujadili utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu. Aidha, nawashukuru wajumbe wa kamati ya PAC na kamati ya bajeti kwa weledi wao waliotuonesha wakati wakifanya kazi nasi. Nawatakia kila la kheri na kuwaahidi kuwa tutakuwa nao pamoja katika kazi zetu na tutaendelea kusikiliza ushauri wao.

7. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue fursa hii kuwashukuru Mawaziri wenzangu, Manaibu Mawaziri na wajumbe wote wa Baraza hili tukufu kwa ushirikiano mnaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Nidhahiri kwamba ushirikiano baina yetu ni nguzo muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa Ilani ya CCM, mipango na mikakati ya kitaifa katika kuleta maendeleo na kukuza uchumi na hali za maisha ya wananchi wa Zanzibar,

8. **Mheshimiwa Spika,** baada ya utangulizi huo, sasa naomba kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na mwelekeo wa malengo na bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kama ifuatavyo:

## B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ilipanga kutekeleza bajeti kwa kuzingatia vipaombele vifuatavyo:-

i. Kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa habari sahihi na kwa wakati kwa wananchi kupitia vyombo vya habari vya umma na binafsi.
ii. Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa vyombo vya habari, uchapaji na utangazaji ili kuhakikisha vinafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya taaluma.
iii. Kutoa huduma za uchapaji na Bohari kuu ya vifaa vya ofisi na kuandikia kwa Taasisi za Serikali na Binafsi;
iv. Kutoa elimu kwa jamii juu ya kulinda mila silka na utamaduni wa mzanzibari na kuwajengea uwezo wajasiriamali wa bidhaa za kiutamaduni;
v. Kusimamia shughuli za Sanaa na Burudani pamoja na kuwaunganisha wasanii na fursa mbali mbali ndani na nje ya nchi;

vi. Kuendeleza, kukuza na kueneza matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu kwa wageni na wenyeji pamoja na kutoa mafunzo ya mbinu za kufundisha Kiswahili;
vii. Kusimamia na kuimarisha miundombinu ya michezo pamoja na kuratibu maendeleo ya michezo kwa kuviwezesha vyama vya michezo kuendesha shughuli zao kwa mujibu wa Sera na Sheria;
viii. Kukamilisha Sera, Sheria na Kanuni za Wizara ambazo zimefanyiwa mapitio ili ziweze kutumika, kufanya ufuatiliaji wa miradi na program pamoja na kufanya tafiti katika Sekta ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo; na
ix. Kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi na wafanyakazi ikiwemo utoaji wa vitendea kazi na stahiki za wafanyakazi kwa mujibu wa sheria na kuwaendeleza kwa kuwapatia mafunzo.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI, 2025 HADI MACHI, 2026

### C.1. Fedha zilizopatikana kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026

10. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kupitia Programu zake kuu Nne (4) zinazotekelezwa katika Fungu J03, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imeidhinishiwa matumizi ya jumla ya **TZS 453,391,093,000/-**. Kati ya fedha hizo **TZS 19,807,111,000/-** ni jumla ya Matumizi ya Kazi za Kawaida (**TZS 14,060,700,000/-** ni mishahara na **TZS 5,746,411,000/-** ni matumizi ya Uendeshaji) na **TZS 433,583,982,000/-** ni jumla ya matumizi ya miradi ya Maendeleo.

11. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 211,962,939,100/-**zimepatikana sawa na asilimia **63** ya makadirio ya bajeti ya kipindi cha miezi tisa na asilimia **47** ya makadirio kwa mwaka. Kati ya fedha hizo, **TZS 12,500,142,804/-** ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia **83** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia

**59** ya makadirio ya mwaka (**TZS 10,088,609,590/-** ni mishahara na **TZS 2,411,533,214/-** ni matumizi ya Uendeshaji) na **TZS 199,462,796,296/-** ni kwa kazi za Maendeleo sawa na asilimia **63** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **46** ya makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho 1A na 1B vinatoa ufafanuzi.**

12. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, kwa upande wa Fungu J05, linalotekeleza Programu moja kuu na programu mbili ndogo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 liliidhinishiwa jumla ya **TZS 1,456,900,000/-** (**TZS 777,500,000/-** ni mishahara na **TZS 679,400,000/**- ni matumizi ya Uendeshaji).

13. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 773,480,558/-** zimepatikana sawa na asilimia **65** ya makadirio ya bajeti ya kipindi cha miezi tisa na asilimia **53** ya makadirio kwa mwaka. **Kiambatanisho 1A na 1B vinatoa ufafanuzi.**

### C.2 Ukusanyaji wa Mapato kwa Kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 710,000,000/-** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 437,640,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 318,437,250/-** zimekusanywa sawa na asilimia **73** ya makadirio kwa kipindi hicho ambayo ni sawa na asilimia **45** ya makadirio ya mwaka. **Kiambatanisho 1C vinatoa ufafanuzi.**

### C.3. Utekelezaji wa Programu za Wizara kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026

15. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo imetekeleza kazi zake kupitia

Programu Kuu Tatu (3) na Programu ndogo Saba (7). Utekelezaji wa Programu hizo kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ni kama ifuatavyo: -

### C.4.1. PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

16. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuongeza upatikanaji na usambazaji wa Habari sahihi na kwa wakati kwa wananchi kupitia Vyombo vya Habari. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu hii ina Programu ndogo mbili (2) ambazo ni Programu ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Programu ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji.

#### C.4.1.1 Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

17. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar (SMS). Wizara kupitia programu ndogo hii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

### IDARA YA HABARI MAELEZO

18. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Habari Maelezo kupitia programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari imepewa jukumu la Kusimamia, Kuratibu na Kusambaza taarifa sahihi za Serikali kwa umma pamoja na kuwaelimisha wananchi kuhusu sera, mipango na mafanikio ya Serikali kupitia vyombo vya habari. Wizara kupitia Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a. **Utoaji wa Taarifa, Picha na Makala:** Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kusambaza katika vyombo vya habari jumla ya taarifa 353 kuuza picha za viongozi wakuu 157 na kuandaa makala 27.

b. **Kuandaa mikutano ya Mawaziri, Wakuu wa Taasisi za SMZ na vyombo vya Habari:** Idara ya Habari imefanikiwa kuratibu kipindi maalum cha mafanikio ya siku 100 za uongozi wa Mhe. Dkt. Mwinyi, ambapo Mawaziri wa Wizara zote walipata fursa ya kuelezea utekelezaji wa majukumu yao kupitia vyombo vya habari ikiwemo ZBC, kwa lengo la kuimarisha uwazi, uwajibikaji na kuwafahamisha wananchi maendeleo yaliyofikiwa katika kutekeleza ahadi za Serikali.

c. **Kufanya Mikutano ya Maafisa Habari:** Idara imefanikiwa kufanya mkutano mmoja na wa maafisa habari na Mawasiliano wa Wizara za SMZ na kuratibu mkutano mmoja wa wanahabari uliojumuisha maafisa habari kutoka Serikali ya ya Mapinduzi ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo ni kuimarisha ushirikiano, kubadilishana uzoefu na kuratibu mtiririko wa habari rasmi za Serikali kwa umma ili kuleta kauli moja katika kusemea mafanikio ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

**Mapato na Matumizi**

**19. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Idara ya Habari Maelezo ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 200,000,000/-** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 121,700,000/-** hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 132,774,75/-** zimekusanywa sawa na asilimia **11** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **7** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 katika programu hii ndogo ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 188,290,000/-** ikiwa ni matumizi ya uendeshaji kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 177,690,000/-.** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 83,830,000/-** zimetumika sawa na asilimia **47** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **45** ya makadirio ya mwaka.

## SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)

20. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utangazaji Zanzibar kupitia programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari ina jukumu la kutoa huduma za utangazaji kwa umma kwa njia ya redio, televisheni na majukwaa ya kidigitali kwa lengo la kutoa habari, kuelimisha na kuburudisha jamii. Wizara kupitia ZBC imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

a. **Kuandaa vipindi na kurusha matangazo ya Televisheni na Redio:** ZBC imeandaa na kurusha hewani vipindi vya ndani 15,921, Vipindi vya nje 322 na matangazo 32,099. Aidha, matangazo yaliyorushwa mubashara ni 408.

b. **Kusimamia na kufuatilia shughuli za masoko na uwekezaji:** ZBC imeongeza juhudi katika kufuatilia masoko ikiwemo kutafuta wadhamini kwa ajili ya mashindano ya Yamle Yamle Cup ambapo jumla ya wadhamini 10 walijitokeza wakiwemo PBZ, Mwanamke Initiative Foundation, ZURA, Zan Aqua, ZRA, ZSTC, Pondeza Foundation na VIGOR. Kupita juhudi hizi Shirika limeweza kukusanya mapato ya ndani shilingi 1,278,841,192/- sawa na asilimia **94** ya makadirio ya **shilingi 1,358,284,500/-.**

c. **Kuratibu shughuli za utawala na usimamizi wa Vituo vya ZBC:** Shirika la Utangazaji (ZBC) limefanikiwa kuratibu na kuimarisha shughuli za utawala na usimamizi kwa kutoa huduma bora za kiofisi na rasilimali watu katika vituo vya Unguja, Pemba, Dodoma na Dar es Salaam, hatua inayolenga kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kuhakikisha huduma za utangazaji zinawafikia wananchi kwa ubora wa hali ya juu nchi nzima.

d. **Kuunganishanakusambazamaudhuikupitiakin’gamuzi cha Bayt**: ZBC imeendelea kusimamia na kuimarisha utoaji wa huduma ya uunganishaji na usambazaji wa maudhui kupitia king’amuzi cha Bayt, ili kupanua wigo wa upatikanaji wa taarifa na burudani kwa jamii kupitia teknolojia ya kisasa inayokidhi mahitaji ya soko la sasa. Vilevile, ZBC imefanya tathmini ya kina ya

utekelezaji wa shughuli zake ambapo ripoti inaonesha mafanikio makubwa katika kusambaza taarifa kwa wakati, kuelimisha, na kuburudisha umma kupitia vipindi mbalimbali vya ubora. Pamoja na mafanikio hayo, Shirika limebaini umuhimu wa kuongeza uwekezaji katika teknolojia za kisasa na kupanua wigo wa usikivu na utazamaji ili kuendana na mabadiliko ya kidijitali na kufikia hadhira kubwa zaidi ndani na nje ya nchi.

**Mapato na Matumizi**

21. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Shirika la Utangazaji Zanzibar lilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 3,300,000,000/-** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 2,250,000,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 2,219,100,259/-** zimekusanywa sawa na asilimia **99** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **67** ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 3,842,900,000/-** ikiwa ni matumizi ya mishahara. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 2,882,175,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 2,505,010,870/-** zimetumika sawa na asilimia **87** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **65** ya makadirio ya mwaka.

## SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI (SMS)

22. **Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) kupitia programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari ina jukumu la kuchapisha na kusambaza magazeti na machapisho mengine kwa lengo la kutoa taarifa kwa umma kuhusu sera, mipango na mafanikio ya Serikali. Wizara kupitia Shirika la Magazeti imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a. **Kuimarisha shughuli za uchapishaji na usambazaji wa gazeti:** Shirika limefanikiwa kuendesha shughuli zake kwa kutumia mapato ya ndani, ambapo limechapisha na kusambaza zaidi ya nakala 917,000 za magazeti ya Zanzibarleo, Zanzibar Mail, na Zaspoti. Wigo wa usambazaji umetanuka kutoka vituo 100 hadi 130 Tanzania nzima. Kuanzishwa kwa mfumo wa e-Magazeti kumesaidia kudhibiti mapato, kuimarisha usalama wa taarifa kulingana na miongozo ya Serikali Mtandao (eGAZ), na kurahisisha upatikanaji wa ripoti za kibiashara. Aidha, Shirika limechapisha zaidi ya habari 10,000, matangazo 2,475, picha 12,871 na makala 800 zinazohusu masuala ya ndani na nje ya nchi. Vilevile, matoleo maalum yameandaliwa kuelezea mafanikio ya Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano, lengo likiwa ni kuelimisha jamii kuhusu historia na maendeleo ya nchi.

b. **Kulitangaza Shirika ili Kwenda kidigitali:** Shirika limeimarisha uwepo wake mtandaoni, ambapo maudhui yake yanasomwa kupitia blogu 12, vituo 9 vya televisheni, na redio 10 nchini. Kupitia mitandao ya kijamii, Shirika limepata wafuasi wengi, hususan TikTok (348,000) na YouTube (36,433) pamoja na kupatikana mtandaoni duniani kote kupitia tovuti yake epapers@smsz.co.tz, jambo linalosaidia kufikisha habari kwa hadhira kubwa zaidi. Katika hatua nyengine, Shirika linaendelea kuweka logo zake katika bahasha ambapo utaratibu unaendelea chini ya usimamizi wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar na hadi sasa jumla ya bahasha 200 tayari zimewekewa logo.

c. **Kuimarisha huduma za kiutawala na uendeshaji wa ofisi:** Shirika limefanya malipo ya huduma mbalimbali za uendeshaji wa ofisi, kulipa stahiki za wafanyakazi pamoja na kuwajengea uwezo wafanyakazi ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Aidha, Shirika la Magazeti lilifanya marekebisho ya rasimu ya mapendekezo ya Sheria mpya baada kujadiliwa katika kikao cha Kamati ya Sheria na Kanuni ya Baraza la Mapinduzi na kupewa maelekezo. Vilevile, vikao viwili vya Bodi vimefanyika kujadili utekelezaji wa shughuli za Shirika

d. **Kuendelea kupata tunzo za kufanya kazi kwa ufanisi pamoja na kutoa mashirikiano:** Shirika la Magazeti ya Serikali kwa mwaka wa Fedha 2025/2026 limefanikiwa kushinda tuzo 9 zinazotolewa na Mashirika na Taasisi za Serikali pamoja na Taasisi za kiraia, kwa lengo la kutambua mchango wake katika kutoa habari sahihi, kuelimisha jamii na kuendeleza sekta ya habari nchini. Mafanikio haya yanajumuisha uandishi bora, uhariri, umahiri, taarifa za uchunguzi pamoja na mawasiliano na yanaonesha juhudi na weledi wa Taasisi katika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**Mapato na Matumizi**

23. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Shirika la Magazeti ya Serikali lilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 1,500,000,000/-** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 1,094,500,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 860,132,581/-** zimekusanywa sawa na asilimia **79** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **57** ya makadirio ya mwaka. Kwa upande wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Shirika lilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 1,587,500,000/-** ikiwa ni matumizi ya mishahara. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 1,190,625,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 931,345,459/-** zimetumika sawa na asilimia **78** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **59** ya makadirio ya mwaka.

**C.4.1.2 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji.**

24. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Habari Maelezo, Tume ya Utangazaji Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar. Jukumu la msingi katika programu ndogo hii ni kudhibiti na kusimamia, waandishi wa habari, Vyombo vya habari, vituo vya utangazaji na kusimamia shughuli za uchapaji.

## IDARA YA HABARI MAELEZO

a. **Kudhibiti na kusimamia shughuli za Habari, kupitia sera na sheria za Habari na Utangazaji:** Idara ya Habari Maelezo imefanikiwa kutoa vibali 6 na vitambulisho vya waandishi wa habari 795 ya makadirio ya miezi tisa.

25. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 katika programu hii ndogo Idara ya Habari Maelezo ilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 1,075,912,033/-** ikiwa ni matumizi ya uendeshaji na mishahara, na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 648,465,500/-** ikiwa ni matumizi ya kawaida. hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 442,100,413/-** zimetumika sawa na asilimia **68** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **41** ya makadirio ya mwaka.

## WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR

26. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Serikali wa Uchapaji kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji ina jukumu la kutoa huduma ya uchapaji wa nyaraka na machapisho rasmi ya Serikali. Aidha, wakala ina wajibu wa kutoa huduma za bohari ya vifaa vya ofisini na kuandikia kwa taasisi za Serikali na Binafsi. Wizara kupitia Wakala wa Uchapaji imetekeleza shughuli zifuatazo:-

a. **Kusimamia shughuli za upigaji chapa:** Wakala wa Serikali wa Uchapaji umepokea na kuchapisha kazi 373 zenye thamani ya TZS 2,768,568,080/- kutoka taasisi za Serikali na binafsi. Kadhalika, Wakala umechapisha magazeti rasmi ya Serikali 113 kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Vilevile, Wakala umechapisha kwa mafanikio mitihani ya darasa la nne kutoka Baraza la Mitihani Zanzibar kazi ambayo ilifanyika kwa ufanisi na usiri mkubwa. Katika kipindi husika, Wakala umefanikiwa kununua Malighafi za uchapishaji zenye thamani ya TZS. Milioni 665,322,720/- ikiwemo

boksi za Diary, Wino, na malighafi za uchapishaji wa kazi mbali mbali.

b. **Kufanya matengenezo ya Mitambo ya uchapaji:** Wakala umefanikiwa kufanya matengenezo makubwa na madogo ya vifaa na mitambo 10 ya uchapaji pamoja na ununuzi wa mtambo wa STICH na mtambo wa kuhesabia karatasi yenye thamani ya jumla ya **TZS. Milioni 68,928,690/-.**Sambamba na hilo, Wakala umefanikiwa kununua SERVER kwa ajili ya kudhibiti mifumo ya ofisi, udhibiti taarifa za uzalishaji na uendeshaji na ripoti muhimu zinazohusu miundo ya kifedha.

c. **Kuimarisha uendeshaji wa bohari kuu:** Wakala umefanya ununuzi ya vifaa vya ofisi na kuandikia vyenye thamani ya **TZS. Milioni 735,414,740/-** kwa kuzingatia mahitaji ya maombi yanayowasilishwa na Taasisi. Ilikadiriwa jumla ya taasisi 102 kuwasilisha maombi ya huduma ya vifaa vya ofisi na kuandikia katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ambapo uhalisia taasisi zilizowasilisha maombi ni 44 sawa na asilimia **43** na maombi yote yameshafanyiwa kazi.

**Mapato na Matumizi**

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wakala wa Serikali wa Uchapaji ulikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 3,607,952,000/-** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 2,900,549,830/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 4,853,371,078/-** zimekusanywa sawa na asilimia **167** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **135** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wakala ulipangiwa kutumia jumla ya **TZS 2,475,300,000/-** ikiwa ni matumizi ya mishahara. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 1,856,475,000/-.** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 1,621,372,434/-** zimetumika sawa na asilimia **87** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 66 ya makadirio ya mwaka.

## TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR

28. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utangazaji Zanzibar inatekeleza Programu kuu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji yenye programu ndogo mbili; Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji na programu ndogo ya Usimamizi wa Rasilimali watu, Utawala na Uendeshaji. Kupitia programu hizo, imetekeleza shughuli zifuatazo: -

a. **Kudhibiti na kusimamia shughuli za utangazaji kupitia Sera na Sheria za Utangazaji**: Tume ya Utangazaji imefanikiwa kuimarisha usimamizi na udhibiti kwa kukagua vituo 37 vya utangazaji Unguja na Pemba, pamoja na kufuatilia maudhui ya redio 18, televisheni nane (8), na vituo20 vya maudhui ya mtandaoni. Katika hatua nyingine ya uratibu, Tume imetoa leseni sita (6) kwa vituo vya maudhui ya mtandaoni na kukamilisha uandaji wa mwongozo wa maombi ya leseni, ambao unatarajiwa kuanza kutumika mara baada ya kuidhinishwa na Bodi.

b. **Kuitangaza Tume ya Utangazaji Zanzibar kwa umma ili kukuza utendaji kazi:** Tume imefanikiwa kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria, kanuni, na miongozo ya utangazaji wakati wa uchaguzi kupitia vikao saba vya wadau na vipindi vya redio Unguja na Pemba. Aidha, uelewa wa jamii umeimarishwa kupitia usambazaji wa jumbe fupi 84 mitandaoni na uchapishaji wa makala mbili katika Gazeti la Zanzibar Leo, zikielezea jukumu la vyombo vya habari katika kulinda amani na nafasi ya Tume katika usimamizi wa sekta.

c. **Kuweka Mazingira bora ya Kazi:** Tume imefanikiwa kufunga mfumo wa kisasa wa kufuatilia maudhui ya redio na televisheni kwa ushirikiano na TCRA ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, sambamba na kuimarisha mazingira ya kazi kupitia mafunzo ya wafanyakazi na utoaji wa stahiki kwa watumishi. Hatua hizi zimeenda sanjari na uratibu wa mikutano ya Bodi ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi iliyolenga usimamizi wa ujenzi wa jengo

la Tume na tathmini ya ripoti za ukaguzi wa ndani kwa mwaka 2024/25.

**Mapato na Matumizi**

29. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Utangazaji Zanzibar imeikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 320,000,000/-** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 311,100,000/-**Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 139,600,000/-** zimekusanywa sawa na asilimia **45** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 44 ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Tume ya Utangazaji ilipangiwa kutumia jumla ya T**ZS 1,456,900,000/-** ikiwa ni matumizi ya kawaida. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 1,182,897,560/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 773,480,558/-** zimetumika sawa na asilimia **65** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **53** ya makadirio ya mwaka.

## C.4.2 PROGRAMU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO.

30. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa Utamaduni, Lugha ya Kiswahili na Sanaa Zanzibar zinaenziwa pia wasanii wanaendelezwa kiuchumi ili kupunguza umaskini na kuifanya michezo kuwa ni sehemu ya kujenga amani, utulivu, ajira pamoja na kujenga afya kwa jamii. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Programu hii ina Programu Ndogo mbili (2) ambazo ni Programu ya Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa na Programu ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo.

### C.4.2.1 Programu Ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa

31. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Utamaduni, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu (BASSFU) na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA). Wizara kupitia programu hii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

**IDARA YA UTAMADUNI**

32. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Utamaduni kupitia programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa imepewa jukumu la Kusimamia, kuendeleza na kukuza maendeleo ya shughuli za utamaduni kwa wananchi.

Idara ya Utamaduni imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

a. **Kuandaa Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari:** Idara ya Utamaduni imefanikiwa kuandaa Tamasha la 30 la Utamaduni wa Mzanzibari Unguja na Pemba, lililowashirikisha wasanii 129 na kuonesha sanaa, vyakula, na michezo ya asili. Tamasha hili lina dhumuni la kuenzi utamaduni wa Mzanzibari na kuimarisha mwamko wa jamii kuhusu maadili ya kitaifa, ikiwemo uvaaji wa mavazi ya asili na yenye staha visiwani humo.
b. **Kutoa elimu ya kulinda na kuendeleza Utamaduni wa Mzanzibari:** Idara imefanikiwa kutoa elimu na kuhamasisha jamii juu ya ulinzi wa Utamaduni wa Mzanzibari na mapambano dhidi ya mmong'onyoko wa maadili kupitia vyombo vya habari, ambapo jumla ya vipindi 50 vimerushwa kupitia televisheni, redio, na magazeti nchi nzima.
c. **Kuviwezesha na kuviendeleza vikundi vya Utamaduni:** Idara imefanikiwa kuviwezesha vikundi mbalimbali vya sanaa na wajasiriamali kwa kuvipatia vifaa vya kazi pamoja na ruzuku ya fedha taslimu kiasi cha shilingi 8,500,000/-. Ufadhili huo

umenufaisha jumla ya vikundi 22 (vikundi 12 vya sanaa na 10 vya wajasiriamali), kwa lengo la kuimarisha utendaji na kufanikisha utekelezaji wa shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

d. **Uimarishaji wa Maadili kupitia Mabaraza ya Wazee:** Idara ya Utamaduni imefanikiwa kurejesha Mabaraza ya Wazee kwa lengo la kupambana na mmong'onyoko wa maadili na kutoa malezi kwa vijana kulingana na misingi ya utamaduni wa Mzanzibari. Hatua hii inalenga kurejesha heshima, mavazi ya staha, na kupunguza vitendo vya uhalifu na unyanyasaji katika jamii kupitia ushauri na miongozo kutoka kwa wazee.

e. **Kuendeleza Mashirikiano na Tasisi za Serikali na Binafsi katika kutunza na kuendeleza Utamaduni za Mzanzibari:** Wizara kupitia Idara ya Utamaduni imeimarisha mashirikiano na taasisi za kiserikali na binafsi, ikiwemo Wizara ya Utalii na Serikali za Mitaa, ili kudhibiti athari za utandawazina utalii dhidi ya maadili ya nchi. Aidha, mazungumzo yamefanyika na wamiliki wa boti za abiria ili kurusha matangazo ya kuelimisha wageni kuhusu utamaduni na kanuni za uvaaji wanapoingia Zanzibar.

**Mapato na Matumizi**

33. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 Idara ya Utamaduni ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 5,851,259,000/- ikiwa ni matumizi ya kawaida na Miradi ya maendeleo. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS5,143,346,750/-**(**TZS2,143,346,750/-**zamatumizi ya kawaida na T**ZS 3,000,000,000/-** ya Miradi ya maendeleo). Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 3,865,453,498/-** (**TZS 1,912,428,360/-** matumizi ya kawaida na **1,953,025,138/-** za miradi ya maendeleo) zimetumika sawa na asilimia **75** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **66** ya makadirio ya mwaka.

## BARAZA LA SANAA NA SENSA YA FILAMU (BASSFU)

34. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu kupitia programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni ina jukumu la kukuza na kuendeleza sanaa na wasanii pamoja na kufanya ukaguzi wa filamu, sanaa na maonesho. Baraza la Sanaa limefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

a. **Kukagua kazi, Taasisi na maeneo ya Sanaa:** Baraza la Sanaa limefanikiwa kufanya ukaguzi katika maeneo 267 yanayojishughulisha na burudani, yakiwemo mahoteli 151, kumbi za starehe 95, na kumbi za burudani 21, ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, kanuni, na taratibu zinazolinda mila, silka, na utamaduni wa Mzanzibari. Aidha, Baraza limehakiki jumla ya kazi za sanaa 275, zikiwemo nyimbo, kasida, na filamu, kwa lengo la kudhibiti maudhui na kuhakikisha kazi hizo zinaakisi maadili ya jamii na kukuza utambulisho wa kitaifa.

b. **Kutoa Mafunzo ya Masoko kwa Wasanii:** Baraza la Sanaa, imefanikiwa kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo wasanii 40 kuhusu mbinu za masoko na ujenzi wa chapa (Branding). Lengo la mafunzo haya ni kuwawezesha wasanii kuzalisha kazi zenye viwango vya ubora na kuwapatia ujuzi wa kutafuta fursa za masoko ya uhakika ndani ya tasnia ya sanaa.

c. **Kuwaenzi na kuwaendeleza wasanii wakongwe:** Baraza la Sanaa imefanikiwa kutoa tuzo kwa wasanii watano (5) mashuhuri kama ishara ya kutambua na kuthamini mchango wao mkubwa uliowacha alama katika tasnia ya sanaa na kuitangaza Zanzibar kimataifa. Wasanii waliotunukiwa ni pamoja na Mzee Sekembuke, Mzee Kheri, na Siti Amina kutoka Unguja, huku kwa upande wa Pemba wakiwa ni Mzee Omari Fadhili (muziki wa kizazi kipya) na Bi Rukia (Taarab asilia). Sambamba na hatua hiyo, Wizara imewatembelea wasanii 13 (Pemba 5 na Unguja 8) kwa lengo la kuwajulia hali, kuimarisha mahusiano, na kuthamini mchango wa wakongwe hao katika kurithisha maadili ya nchi kupitia sanaa.

d. **Kuhamasisha wasanii kusajili kazi zao:** Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu, limefanikiwa kutoa elimu kwa wasanii na jamii kupitia kurushwa kwa vipindi 78 vya redio na televisheni vilivyolenga kuhamasisha usajili wa wasanii na kazi zao. Hatua hiyo imekwenda sambamba na mikutano ya kijamii katika shehia mbalimbali za Unguja na Pemba, kwa lengo la kutoa taaluma kuhusu ulinzi wa maadili, mila, na desturi za Zanzibar ili kuhakikisha sanaa inatumika kama nyenzo ya kuimarisha utambulisho wa kitaifa.

**Mapato na Matumizi**

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu Zanzibar lilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 360,000,000/-** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 233,000,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 279,524,000/-** zimekusanywa sawa na asilimia **120** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **78** ya makadirio ya mwaka.

36. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 Baraza la Sanaa na Sensa Ya Filamu lilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 691,000,000/-** ikiwa ni matumizi ya uendeshaji. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 591,609,481/-** hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 175,459,321/-** zimetumika sawa na asilimia **30** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia 25 ya makadirio ya mwaka.

**BARAZA LA KISWAHILI ZANZIBAR (BAKIZA)**

37. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) kupitia programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni lina jukumu la kukuza na kuendeleza lugha ya Kiswahili pamoja na kutoa elimu ya matumizi fasaha na sanifu ya Lugha ya

Kiswahili. Wizara kupitia Baraza la Kiswahili imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

a. **Kuandaa na kuratibu Makongamano ya Kiswahili:** katika kuendeleza lugha ya Kiswahili Wizara kupitia Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) imefanikiwa kuandaa Kongamano la Tisa la Kiswahili la Kimataifa kwa kuwasilisha makala, kuandaa maonesho, usiku wa Mswahili na ziara ya kitalii. Jumla ya wadau 240 walishiriki katika kongamano hilo kutoka nchi za Komoro, Kenya, Uturuki, China, Marekani, Ufaransa, Sweden, Tanzania bara na wenyeji Zanzibar. Mada kuu ya kongamano ilikuwa Matumizi ya Kiswahili katika Mawasiliano na Maarifa

b. **Kuadhimisha siku ya Kiswahili Duniani:** BAKIZA kwa ushirikiano na BAKITA, imefanya Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani tarehe 7 Julai 2025, yaliyopendezeshwa na shughuli za kitaaluma na kiutamaduni ikiwemo Usiku wa Hazina, makongamano, na utoaji wa Tuzo za Rais kwa washindi wa insha na taasisi bora. Maadhimisho haya yamelenga kuunganisha wadau na wataalamu wa ndani na nje ya nchi katika juhudi za kukuza, kuendeleza, na kudumisha matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu duniani.

   Aidha, BAKIZA kwa ushirikiano na Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki (KAKAMA), imefanikiwa kuadhimisha miaka kumi tangu kuanzishwa kwa Kamisheni hiyo. Maadhimisho hayo yalihusisha uwasilishaji wa mada za kihistoria na makala maalum zinazoangazia mafanikio na safari ya KAKAMA katika kipindi cha muongo mmoja.

c. **Kutoa mafunzo ya ufundishaji wa Kiswahili:** BAKIZA, limeendelea kuimarisha mikakati ya kukibidhaisha Kiswahili kwa kutoa mafunzo ya mbinu za ufundishaji kwa wageni kwa wataalamu 10 kutoka vyuo vikuu na asasi zisizo za kiserikali, ili kunufaika na fursa za ufundishaji ndani na nje ya nchi. Aidha, jumla ya wanafunzi 158 wa sekondari Unguja na Pemba wamejengewa uwezo wa uandishi wa insha, huku waandishi wa habari 75 kutoka

vyombo 17 wakipatiwa mafunzo ya matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu ili kuimarisha viwango vya utangazaji na uandishi nchini.

d. **Kuratibu, kusambaza na kutoa elimu ya matumizi ya Kiswahili:** Baraza la Kiswahili la Zanzibar limeendelea kuimarisha matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu ndani na nje ya nchi kwa kurusha jumla ya vipindi 45 vya habari na vibango (posters) 58 katika mitandao ya kijamii. Juhudi hizi zimelenga kutoa taaluma ya msamiati sahihi, kutangaza machapisho ya Baraza, kukusanya maoni ya wadau kuhusu msamiati mpya, pamoja na kupongeza mafanikio ya Miaka 62 ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia lugha adhimu ya Kiswahili.

e. **Kuhariri nyaraka mbalimbali kwa Lugha ya Kiswahili:** BAKIZA limefanya uhariri na kutafsiri nyaraka muhimu, ikiwemo mradi wa elimu kwa wasichana (Room to Read), muongozo wa uandishi wa vitabu, pamoja na machapisho ya 'Zanzibar ya Dkt. Mwinyi' na 'Je, ni halali kweli'. Lengo la hatua hizi ni kusahihisha makosa ya kilugha na kiufundi ili kuhakikisha maandiko yanayotolewa yanakuwa na taarifa sahihi, sanifu, na zenye kuaminika.

**Mapato na Matumizi**

38. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Baraza la Kiswahili Zanzibar lilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 50,000,000/-** na kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026 ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 40,000,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 10,933,500/-** zimekusanywa sawa na asilimia **27** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **22** ya makadirio ya mwaka.

Kwa upande wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Baraza lilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 353,100,000/-** ikiwa ni matumizi ya uendeshaji wa shughuli za Ofisi. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilikadiriwa kutumia **TZS 301,912,500/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 165,852,173/-**zimetumika sawa na asilimia **55** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **50** ya makadirio ya mwaka.

**Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa Mwanakwerekwe**

39. **Mheshimiwa Spika,** mradi wa ujenzi wa nyumba ya sanaa uliopo Mwanakwerekwe ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 na Kampuni ya Scanic Construction Ltd. Mradi huu umejumuisha ujenzi wa jengo la ghorofa tatu (G+3), ambalo lina kumbi za mafunzo, maonesho na ofisi. Utekelezaji wa mradi umekamilika katika hatua ya ujenzi na hatua nyengine iliyobaki ni ununuzi wa samani na vifaa mbalimbali kwa ajili ya chuo cha sanaa. Kupatikana kwa samani na vifaa kutakiwezesha chuo kuanza kutoa mafunzo ya vitendo na kitaalamu katika fani mbalimbali za sanaa ikiwemo uchongaji, udarizi, ufumaji, ushonaji, mafunzo ya TEHAMA pamoja na utengenezaji wa batiki, hali itakayochangia kukuza ajira, ubunifu na uchumi wa ubunifu nchini.

**C.4.2.2 : Programu Ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo**

40. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa shughuli za Michezo inaundwa na Idara ya Michezo Zanzibar na Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ).

**IDARA YA MICHEZO ZANZIBAR**

41. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Michezo kupitia programu ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo imepewa jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera ya michezo pamoja na kusimamia maendeleo ya miundombinu ya michezo nchini. Wizara kupitia Idara ya Michezo imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo; -

a. **Kusaidia na kuziwezesha timu za Taifa kushiriki katika mashindano ya Kimataifa:** Idara ya Michezo imefanikisha ushiriki wa Chama cha Triathlon katika Mashindano ya Afrika (World Triathlon Development Regional Cup) yaliyofanyika Kilifi,

nchini Kenya mwezi Novemba 2025. Vilevile, Timu ya Taifa ya Wanawake ya mchezo wa Kabaddi iliwezeshwa kushiriki Mashindano ya Dunia nchini Bangladesh, ambapo kati ya nchi 11 zilizoshiriki, Zanzibar ilishika nafasi ya saba (7). Mafanikio haya ni kielelezo cha ukuaji wa michezo nchini na dhamira ya Serikali katika kuimarisha diplomasia ya michezo kimataifa.

b. **Kuandaa mashindano ya Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikal**i: Idara imefanikisha uandaaji wa mashindano ya Mawizara, Mashirika, na Taasisi za Serikali yaliyoshirikisha taasisi 28 (23 kutoka Unguja na 5 kutoka Pemba), ambapo Wizara ya Maji, Nishati na Madini iliibuka bingwa wa mpira wa miguu. Mashindano haya yamechangia kuimarisha afya za watumishi, kujenga mshikamano, na kuibua vipaji maeneo ya kazi. Sambamba na hayo, Wizara imeratibu kwa mafanikio Mashindano ya NMB Mapinduzi Cup 2026 yaliyoshirikisha timu tisa kutoka Tanzania Bara, Zanzibar na Uganda, ambapo Klabu ya Young Africans ilitawazwa kuwa bingwa.

c. **Kuwawezesha Maafisa wa Idara, Viongozi wa Vyama vya Michezo, Waamuzi na Makocha kushiriki Mafunzo ya Kimataifa:** Idara ya Michezo imefanikisha kuwajengea uwezo watendaji wa michezo kwa kugharamia ada ya ushiriki wa kocha mmoja katika mafunzo ya ukocha wa mpira wa miguu yaliyofanyika Mnyanjani, Tanga. Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kuanzia tarehe 15 hadi 24 Desemba, 2025, ni sehemu ya mkakati wa Wizara wa kuimarisha utaalamu na weledi miongoni mwa makocha, waamuzi, na viongozi wa vyama vya michezo nchini.

d. **Kuhamasisha Afya ya Jamii kupitia Michezo:** Wizara kupitia Idara ya Michezo kwa mashirikiano na Chama cha Mazoezi ya Viungo Zanzibar (ZABESA), iliandaa Bonanza la Kitaifa la mazoezi ya viungo tarehe 1 Januari, 2026. Bonanza hilo lilifanikiwa kuwakutanisha washiriki 5,150 kutoka vyama vya mazoezi 151 (Unguja 96, Pemba 41, na Tanzania Bara 14), likiwa na lengo la kuhamasisha utamaduni wa kufanya mazoezi ili kujikinga na

maradhi yasiyoambukiza na kuimarisha afya bora kwa wananchi wote.

**Mapato na Matumizi**

42. **MheshimiwaSpika,**kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Idara ya Michezo ilipangiwa kutumia jumla ya T**ZS 414,581,696,967/-** ikiwa ni matumizi ya Uendeshaji na miradi ya maendeleo. (**497,714,967/-** uendeshaji na **414,083,982,000/-**miradi ya maendeleo) Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 339,184,667,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 195,578,947,858/-** (**296,790,000/-** ni za uendeshaji na **195,282,157,858/-** za miradi ya maendeleo) zimetumika sawa na asilimia **58** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **47** ya makadirio ya mwaka.

**BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO ZANZIBAR (BTMZ)**

43. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ) kupitia program ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo imepewa jukumu la kusimamia na kusajili vyama vya michezo pamoja na kuendeleza na kuratibu maendeleo ya michezo nchini. Wizara kupitia Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo; -

a. **Kusaidia vyama vya Michezo kuandaa na kushiriki mashindano mbalimbali:** Wizara, kupitia Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ), imefanikiwa kuviwezesha vyama kumi (10) vya michezo kuandaa na kushiriki mashindano mbalimbali nchini. Mafanikio hayo ni pamoja na uandaaji wa Ligi Kuu ya Netiboli na Ligi ya Muungano, mashindano ya 'Mr. Zanzibar' (Bodybuilding), Ligi ya Mpira wa Wavu (Volleyball), pamoja na mashindano ya kuhamasisha mchezo wa ngumi (Kickboxing) kisiwani Pemba. Aidha, kwa ushirikiano na Shirikisho la Riadha, Baraza limewezesha

mashindano ya riadha kwa wanawake yaliyofanyika Dar- es -Salaam, ikiwa ni hatua ya kuimarisha ushindani na kuibua vipaji katika michezo mbalimbali.

b. **Kufanya Mikutano na vyama na Vilabu vya Michezo:** Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ) limeliwezesha Shirikisho la Mchezo wa Ngumi nchini kuendesha mafunzo maalum ya kuwajengea uwezo wanamichezo chini ya wakufunzi kutoka nchini Brazil, kwa lengo la kuongeza ujuzi na mbinu za kisasa za ulingoni. Vilevile, Baraza limesimamia na kusaidia uratibu wa chaguzi za kidemokrasia kwa vyama vitatu vya michezo ambavyo ni Shirikisho la Kabaddi, Chama cha Mazoezi ya Viungo (ZABESA), na Chama cha Mpira wa Wavu (Volleyball), hatua iliyopelekea kupatikana kwa viongozi wapya watakaoviongoza vyama hivyo kwa ufanisi.

d. **Kuhamasisha Jamii kushiriki katika Michezo kwa kuandaa Mashindano ya ndani na kitaifa**: Vilevile, katika juhudi za kuimarisha na kukuza michezo ya asili na kijamii, Baraza limefanikisha uandaaji wa mashindano ya Karata, Bao, na Dhumna. Mashindano hayo yalifanyika wakati wa Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari huko Kiboje, Wilaya ya Kati, yakiwa na lengo la kuhifadhi michezo ya jadi na kuimarisha utambulisho wa kitaifa.

e. **Kuviwezesha vyama vya michezo vya Watu Wenye Ulemavu kushiriki katika Michezo:** Kwa upande wa michezo ya watu wenye ulemavu, Baraza limesaidia Chama cha Michezo ya watu wenye Ulemavu wa Mguu/mkono mmoja (Amputee) kuandaa mashindano ya michezo ya watu wenye Ulemavu kwa lengo la kuhamasisha watu wenye ulemavu kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 Zanzibar.

### Mapato na Matumizi

44. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Baraza la Taifa la Michezo lilipangiwa kutumia jumla ya **TZS 350,500,000**

ikiwa ni matumizi ya uendeshaji. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 271,490,000/-**Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 105,437,811/-** zilitumika sawa na asilimia **39** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **30** ya makadirio ya mwaka.

## URATIBU WA MASHINDANO YA CHAN 2024

**45. Mheshimiwa Spika,** mashindano ya Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) 2024 yaliyofanyika mwezi Agosti 2025, yalitumika kama kipimo muhimu cha utayari wa Zanzibar kuelekea AFCON 2027. Katika kipindi hicho, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo iliratibu utekelezaji wa shughuli muhimu kupitia kamati ndogo 13, ikijumuisha uimarishaji wa miundombinu ya viwanja kukidhi matakwa ya CAF na ufungaji wa mifumo ya kisasa ya TEHAMA, CCTV, na VOC katika uwanja wa New Amaan Complex. Aidha, Serikali ilifanikiwa kutekeleza makubaliano ya kisheria (Government Guarantee) kwa kutoa misamaha ya kodi, bima za afya na kuondoa ada za viza kwa wageni, huku ikisimamia ugawaji wa tiketi 45,404 na ununuzi wa vifaa vya kiofisi vitakavyotumika pia katika maandalizi ya AFCON 2027.

**46. Mheshimiwa Spika,** uendeshaji wa mashindano ya Kundi D hapa Zanzibar ulipata mafanikio makubwa kwa kuwa kituo pekee ambacho hakikutozwa faini yoyote na CAF kwa kipindi chote cha michuano. Mafanikio haya yameleta tija pana kwa nchi, ikiwemo kuitangaza Zanzibar kimataifa kupitia masoko ya kidijitali na kuwajengea uwezo wa kitaalamu watendaji wetu wa ndani pamoja na vijana wa kujitolea 382. Vilevile, mashindano haya yalitoa fursa za kiuchumi kwa sekta ya utalii na huduma kupitia matumizi ya hoteli na usafiri kwa timu na wageni wa kimataifa, jambo ambalo limeweka msingi madhubuti wa kitalii na michezo kwa siku zijazo.

47. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na ukweli kuwa maandalizi ya AFCON ni jambo mtambuka, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, ikiwa mratibu mkuu, inatoa wito wa dhati kwa sekta zote ikiwemo Ulinzi, Afya, Miundombinu na Utalii kuimarisha ushirikiano kuanzia hatua za awali za upangaji wa bajeti ya mwaka 2026/2027. Ushirikiano huu ni muhimu katika kuhakikisha miundombinu iliyokamilika inatunzwa, miongozo ya CAF inazingatiwa kikamilifu na rasilimali zinapatikana kwa wakati ili kuepuka changamoto za kifedha zilizojitokeza awali. Ni muhimu kwa taasisi za Serikali na sekta binafsi kuungana ili kuendeleza mafanikio yaliyopatikana wakati wa CHAN na kuhakikisha Zanzibar inakua kituo bora kitakachoendesha mashindano ya AFCON yenye viwango vya juu zaidi vya kimataifa.

48. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa gharama, bajeti ya TZS **Bilioni 2,900,000,000/-** ilipangwa kwa ajili ya mashindano ya CHAN Zanzibar, ambapo jumla ya **TZS 2,734,845,120/-** ilipokelewa na kutumika. Fedha hizi zilitumika katika mafungu makuu matatu: ununuzi wa vifaa (34.6%), utoaji wa huduma (27.8%), na maslahi ya wafanyakazi 872 walioshiriki katika operesheni za mashindano (37.5%).

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### a. Mradi wa ujenzi wa Mji wa Michezo Fumba

49. **Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo inatekeleza mradi wa kimkakati wa ujenzi wa mji wa michezo katika eneo la Fumba – Zanzibar. Wizara imeingia makubaliano na Kampuni ya ORKUN GROUP ZANZIBAR kwa mkataba wa Usanifu na Ujenzi, ambapo mradi utagharimu jumla ya USD 150,000,000 kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hadi sasa Dola za kimarekani milioni 34.0 sawa na asilimia 22.6 ya gharama za mradi zimetumika. Wigo wa Mradi utahusisha Uwanja mkuu utakuwa na uwezo wa kuchukua watazamaji 36,500, viwanja viwili vya mazoezi vyenye uwezo wa

kuchukua watu 10,000 kwa pamoja. Kati ya viwanja hivyo, kimoja kitakuwa na njia za riadha (running track) na kingine kitakuwa na eneo maalum la gwaride (parade square).

Aidha, kutajengwa eneo kubwa la mashabiki (fan zone) nje ya uwanja kwa ajili ya burudani na shughuli mbalimbali, pamoja na bandari ndogo ya teksi za baharini ili kurahisisha usafiri wa majini. Vilevile, mradi utahusisha ujenzi wa bwawa la kuogelea la mita 50 lenye viwango vya kimataifa (Olympic standard), bwawa la kupiga mbizi (diving pool) lenye hadhi ya kimataifa pamoja na Ujenzi wa miundombinu ya eneo zima la mradi.

50. **Mheshimiwa Spika,** mradi huu umeanza Julai 2025 na unatarajiwa kukamilika Disemba 2026. Utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 47 huku kazi mbalimbali zikiendelea kufanyika ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya kimuundo, uchimbaji na maandalizi ya ardhi, ujenzi wa huduma za msingi (infrastructure) pamoja na usakinishaji wa mifumo ya maji.

### b. Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Mikoa na Wilaya

51. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na ujenzi wa Viwanja vya Mikoa na Wilaya za Unguja na Pemba unaotekelezwa na Kampuni ya 'Reform Sport' kwa makubaliano ya mkataba wa usanifu na ujenzi. Wigo wa mradi umehusisha ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwemo 'Maisara sports complex', viwanja viwili vya daraja la kwanza (Type 1), viwanja vitatu vya daraja la pili (Type 2), viwanja kumi vya daraja la tatu (Type 3), pamoja na kiwanja kimoja cha daraja la nne (Type 4). Kwa ujumla, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 90. **Kiambatanisho no 1I kinafafanua.**

### c. Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani Pemba

52. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani ulianza utekelezaji wake katika mwaka wa fedha 2024/2025 na

Mkandarasi Kampuni ya ‘Reform Sports’ ya nchini Uturuki. Wigo wa mradi ulijumuisha kazi mbalimbali za ukarabati na ujenzi, ikiwemo ujenzi wa uzio wa ukuta unaozunguka eneo lote la uwanja, ukarabati wa vyumba vya viongozi mashuhuri, ukarabati wa vyumba vya kubadilishia nguo kwa wachezaji, pamoja na ukarabati wa maeneo ya mapokezi ndani na nje ya jengo. Vilevile, umehusisha ujenzi wa jukwaa la viongozi mashuhuri, jukwaa la waandishi wa habari, pamoja na ujenzi wa paa linalofunika eneo la watazamaji na ufungaji wa viti vya kisasa kwa watazamaji.

53. **Mheshimiwa Spika,** Sambamba na hayo, mradi umehusisha ukarabati wa sehemu ya kuchezea mpira (pitch base), uwekaji wa nyasi bandia, uwekaji wa magoli pamoja na uwekaji wa ubao wa kielektroniki. Aidha, utekelezaji wa mradi umekamilika na tayari umeshazinduliwa rasmi mwezi Januari 2026 na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, katika maadhimisho ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

### C.4.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA ZA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO

54. **Mheshimiwa Spika,** programu hii inaundwa na program ndogo tatu ambazo ni program ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Sekta za Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara pamoja na programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango Ofisi Kuu Pemba.

#### C.4.3.1 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo

55. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ina lengo la kuratibu na kusimamia shughuli za utawala na uendeshaji wa ofisi katika Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Programu inatekelezwa

na Idara ya Uendeshaji na Utumishi ambapo kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026, imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

a. **Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Wizara kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi:** Idara ya Uendeshaji na Utumishi imefanikiwa kusimamia na kuratibu mafunzo ya muda mrefu na mafunzo ya muda mfupi ya fani na ngazi tofauti, ndani na nje ya nchi kwa wafanyakazi wa Wizara na Taasisi zake. Kiambatisho No 1J kinafafanua.
b. **Kuimarisha shughuli za Kiutawala na Uendeshaji wa Ofisi:** Idara ya Utumishi imeendelea kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi wake ikiwemo kuwapatia stahiki, vitendea kazi, matengenezo ya jengo na vipando. Aidha, Idara imeendelea kuwafanyia tathmini ya utendaji kazi wafanyakazi pamoja na kuwapatia nyongeza za mwaka ya mishahara, kuwapandisha madaraja wafanyakazi, kuwapanga na kuwasimamia wafanyakazi waliomaliza masomo kuhakikisha wanatumika kwa mujibu wa fani zao. Vilevile, Idara imeratibu na kusimamia ziara za viongozi wakuu wa Wizara upokeaji wa wageni wa ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali.
c. **Kusimamia vitengo vya Wizara:** Idara imeendelea kusimamia kitengo cha ununuzi, uhasibu, mkaguzi wa ndani, kitengo cha habari na Mawasiliano, Kitengo cha Tehama na kitengo cha Sheria kwa lengo la kuleta ufanisi katika utekelezaji wa kazi zao.

**Mapato na Matumizi**

56. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliidhinishiwa jumla ya **TZS 2,437,168,000/-** ikiwa ni matumizi ya kawaida. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 1,901,798,102/-**Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 1,795,159,816/-** zilitumika sawa na asilimia **94** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **74** ya makadirio ya mwaka.

### C.4.3.2 Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

57. **Mheshimiwa Spika,** program ndogo hii ina lengo la kuratibu na kusimamia mipango katika Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, program ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

a. **Kutayarisha Mipango ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:** Wizara imefanikiwa kutayarisha mpango mkakati wa miaka mitano, mpango wa utekelezaji wa mwaka mmoja, mpango wa matumizi (MTEF) wa muda wa kati, kutayarisha na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, Wizara imetayarisha hotuba ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

b. **Kufanya Tafiti katika Sekta za Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo**: Idara ya Mipango imefanikiwa kufanya utafiti kuhusu Utamaduni Uliojificha katika jamii ya kizanzibari. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa utamaduni uliojificha Zanzibar unajidhihirisha kupitia vipengele mbalimbali kama mila zisizoandikwa, mitazamo ya kijamii, ushawishi wa mitandao ya kijamii, pamoja na mabadiliko ya mienendo ya vijana mijini na vIjijini. Imeonekana kuwa utamaduni uliojificha una mchango mkubwa katika kuunda upya utambulisho wa jamii ya Zanzibar, hasa kwa vijana wanaoathiriwa na utandawazi, huku wazee wakionesha msimamo wa kulinda utamaduni asilia. Aidha, utamaduni uliojificha una umuhimu fulani katika maisha ya kila siku, lakini unahitaji kuongozwa na miongozo ya maadili ili kulinda utambulisho wa Kizanzibari.

c. **Kuandaa Sera za Sekta za Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo:** Idara ya Mipango imefanikiwa kukamilisha rasimu ya Sera ya Utamaduni Zanzibar 2026 na kupata maoni kutoka kwa Kamati ya Sera na Sheria ya Baraza la Mapinduzi na baada ya kukamilika inategemewa kuzinduliwa rasmi. Aidha, Idara

imefanikiwa kukusanya maoni ya rasimu ya Sera ya Lugha ya Kiswahili na rasimu ya Sera ya Sanaa Zanzibar kutoka kwa wadau mbalimbali Unguja na Pemba. Kwa sasa rasimu za sera zote mbili zipo katika hatua ya kujadiliwa na Kamati Tendaji na Kamati ya Uongozi ya Wizara na hatimaye kupelekwa Serikalini kwa ajili ya maamuzi ya mwisho.

d. **Kufanya Ufuatiliaji, Tathmini na Usimamizi wa Miradi:** Idara ya Mipango imeendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu wa shughuli za programu na miradi ya maendeleo kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji unazingatia mipango, bajeti na viwango vilivyowekwa. Ufuatiliaji huo umehusisha ziara za mara kwa mara katika maeneo ya miradi, ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji, pamoja na kufanya vikao vya tathmini na wadau mbali mbali. Aidha, Idara imebaini changamoto zinazojitokeza na kuchukua hatua stahiki na kuzitatua kwa wakati, ikiwa ni pamoja na kutoa maelekezo ya kitaalamu na kuimarisha usimamizi. Hatua hizi zimechangia kuongeza uwajibikaji, ufanisi na kuhakikisha malengo ya programu na miradi yanafikiwa kwa wakati uliopangwa.

e. **Uratibu wa Shughuli za Kamati za Baraza la Wawakilishi:** Wizara kupitia Idara ya Mipango Sera na Utafiti kwa kipindi cha Julai hadi machi 2025/2026 imefanikiwa kuratibu ziara moja (Pemba) ya kutemebelea viwanja vya michezo kwa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Pia, vikao vitatu (viwili Kamati ya Ustawi wa Jamii na kimoja kamati ya PAC) vimeratibiwa. Lengo la ziara na vikao hivi vya Kamati ni kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali sambamba na kutoa maoni, ushauri na mapendekezo kwa uongozi na watendaji katika kufanikisha malengo ya Wizara.

## MAPATO NA MATUMIZI

**58. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliidhinishiwa jumla ya **TZS**

**315,800,000/-** ikiwa ni matumizi ya kawaida. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 258,214,000/-** Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 110,000,000/-** zilitumika sawa na asilimia **42** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **35** ya makadirio ya mwaka.

#### C.4.3.3 Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango Mikuu ya Ofisi Kuu Pemba

59. **Mheshimiwa Spika,** program ndogo hii ina lengo la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba, program ndogo hii inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -.

a. **Kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programu na Miradi:** Ofisi Kuu Pemba imefanikiwa kuratibu na kusimamia utekelezaji wa program na miradi mbalimbali kwa ufanisi ikiwemo uratibu wa shughuli za utafiti, kuandaa na kuratibu tamasha la utamaduni wa mzanzibar, kuratibu ukusanyaji maoni ya wadau katika mchakato wa maoni ya sera. Aidha Ofisi imeratibu vikao na ziara za Baraza la Wawakilishi kwa lengo la kuimarisha usimamizi na uwajibikaji wa shughuli za Wizara. Vile vile, imeendelea kusimamia miradi ya maendeleo kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu, kutoa miongozo ya kitaalamu na kuhakikisha miradi hio inatekelezwa kwa kuzingatia malengo yaliyowekwa.

b. **Kuimarisha huduma za Kiutawala na Uendeshaji wa Ofisi:** Ofisi kuu Pemba imeweza kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuwapatia wafanyakazi huduma na vitendea kazi, kuwajengea uwezo kitaaluma, kulipa stahiki pamoja na kusimamia nidhamu kazini. Aidha, ofisi imefanikiwa kununua kifaa cha kurikodi mahudhurio ya wafanyakazi (BioMetric) sambamba na kufanya vikao vya kamati tendaji na vikao vya Wafanyakazi kwa ujumla.

## MAPATO NA MATUMIZI

60. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi Kuu Pemba ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 100,000,000,** Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kukusanya TZS 82,900,000/-Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 14,705,000/-** sawa na asilimia **18** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **15** ya makadirio ya mwaka.

61. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba inatekelezwa na Ofisi Kuu Pemba. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, programu ndogo hii iliidhinishiwa jumla ya **TZS 1,376,614,000/-** kwa kazi za kawaida. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 ilipangiwa kutumia **TZS 674,497,102/**-Hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya **TZS 990,446,698/-** zilitumika sawa na asilimia **147** ya makadirio ya miezi tisa na asilimia **72** ya makadirio ya mwaka.

### C.4.4. PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIJANA

62. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina lengo la kuwawezesha Vijana kiuchumi, kijamii na kifikra ili waweze kujitegemea na kuchangia Maendeleo ya Taifa. Programu hii ilikuwa na Programu moja ndogo ambayo ni Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana. Aidha, Programu inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana na Baraza la Vijana Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iliidhinishiwa bajeti ya **TZS 18,260,502,690/-.** Kati ya hizo **TZS 1,760,502,690/**- ni matumizi ya kazi za kawaida na **TZS 16,500,000,000/-** ni matumizi ya kazi za maendeleo.

63. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026 jumla ya **TZS 3,019,041,891/-** zimepatikana sawa na asilimia **17**, kati ya hizo **TZS 791,428,591/-** ni matumizi ya kawaida na **TZS 2,227,613,300/-** ni matumizi ya kazi za Maendeleo.

64. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imehamishiwa katika Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji baada ya muundo mpya wa Mawizara uliofanyika Novemba 2025. Aidha, mafanikio, changamoto na shughuli mbalimbali zilizotekelezwa kupitia programu hii zitawasilishwa na Wizara husika.

### C.5Mafanikio na Changamoto za Wizara kwa Kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026

#### C.5.1 Mafanikio

65. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026, Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo kuongezeka kwa ubora na kasi ya huduma za uchapaji; kuongezeka kwa maombi ya wateja wanaohitaji huduma ya uchapaji na huduma ya vifaa vya ofisi na kuandikia; kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya kijamii na maendeleo kupitia vyombo vya habari; kuongezeka kwa habari muhimu za ndani na nje ya nchi; kuongezeka kwa vipindi na maudhui ya habari.

66. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio mengine ni kuimarika kwa mshikamano wa kitaifa kupitia matukio ya kijamii yaliyoandaliwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar kama vile Yamle Yamle Cup, Iftar na mashindano ya Kimataifa ya kuhifadhi Qur’ani Tukufu sambamba na kuongezeka kwa mapato ya ZBC kupitia matangazo mbalimbali kutokana na kuimarika kwa imani ya wadau. Aidha, Wizara kupitia Shirika la Magazeti ya Serikali imefanikiwa kuongeza nakala za machapisho na usambazaji wa magazeti uliotokana na kupanuka kwa mtandao wa usambazaji kupitia ongezeko la vituo na mawakala wa magazeti kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara. Kadhalika, uwepo wa mfumo wa E-Magazeti umeimarisha usimamizi wa mapato na ufanisi wa shughuli za magazeti.

67. **Mheshimiwa Spika,** usimamizi na ufuatiliaji wa vituo vya utangazaji pamoja na matumizi ya masafa ya FM umeendelea kuimarishwa kupitia matumizi ya mfumo maalum wa ufuatiliaji, sambamba na kufanyika kwa ukaguzi wa mara kwa mara katika vituo vya utangazaji vya Unguja na Pemba. Hatua hii imechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha ufanisi wa utoaji wa huduma za utangazaji pamoja na kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, kanuni na miongozo ya sekta ya utangazaji.

68. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuimarisha uelewa wa wananchi pamoja na wadau mbalimbali kuhusu umuhimu wa kuhifadhi, kuuenzi na kuendeleza utamaduni wa Mzanzibari, hatua ambayo imeendelea kulinda na kudumisha utambulisho wa taifa. Aidha, ushiriki wa wazee kupitia Mabaraza ya Wazee umeendelea kuwa nguzo imara katika kurithisha mila, desturi na silka njema kwa vizazi vya sasa na vijavyo. Hali kadhalika, Wizara imeimarisha ushirikiano kati ya Serikali na wadau mbalimbali, jambo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa kukabiliana na changamoto zinazoathiri maadili ya jamii.
Hivyo basi, napenda kutoa wito kwa jamii kwa ujumla kuendelea kuthamini, kulinda na kuenzi tunu za mila, desturi na maadili mema ya Kizanzibari, ili kudumisha utambulisho wetu wa asili na kuijenga jamii yenye nidhamu, heshima na mshikamano. Ni jukumu la kila mmoja wetu kuwa balozi mzuri wa utamaduni wetu kwa vitendo, hususan kwa kizazi kipya ambacho ndicho tegemeo la taifa letu. Kwa kufanya hivyo, tutahakikisha kuwa urithi wetu wa kitamaduni unaendelea kuishi na kunufaisha kizazi cha sasa na kijacho.

69. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanikiwa kuzindua programu ya ubunifu wa kimkakati kwa wasanii yenye lengo la kuimarisha ujuzi na ubunifu wa wasanii, kuongeza fursa za ajira na kipato, pamoja na kukuza ushindani wa kazi za sanaa katika soko la ndani na la kimataifa kwa maendeleo endelevu ya sekta ya sanaa na utamaduni. Vilevile, kupitia programu na juhudi mbalimbali za uhamasishaji,

Wizara imeendelea kuimarisha matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu na fasaha, kuongeza uelewa wa jamii kuhusu umuhimu wa lugha hiyo na kuchochea matumizi yake katika nyanja rasmi na zisizo rasmi. Mafanikio haya yamechangia kuongezeka kwa hadhi ya Kiswahili ndani ya nchi na kuimarika kwa ushawishi wake kimataifa, hatua inayothibitisha mchango mkubwa wa Wizara katika kukuza utamaduni na lugha kama nyenzo ya maendeleo na utambulisho wa taifa.

70. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026, Wizara imeanza maandalizi rasmi ya Mashindano ya AFCON 2027 kwa kuanza ujenzi wa Mji wa Michezo katika eneo la Fumba Zanzibar. Ujenzi huo unaojumuisha uwanja wa kisasa wenye uwezo wa kubeba watazamaji 36,500, hatua inayotarajiwa kuimarisha hadhi ya Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ikiwemo AFCON 2027. Aidha, ukarabati wa viwanja vya Amaan, Gombani na Mao Zedong umekamilika kwa mafanikio makubwa sambamba na kufikia hatua za mwisho za ujenzi wa viwanja vya michezo vya Mikoa na Wilaya. Katika hatua nyengine, Wizara imefanikiwa kuongeza ushiriki wa michezo ya kimataifa kupitia vyama vya michezo mbalimbali. Miongoni mwa vyama vilivyopata fursa ya kushiriki kimataifa ni Chama cha Riadha kilichoshiriki Mashindano ya Vijana chini ya umri wa miaka 17 yaliyofanyika Luanda nchini Angola; Chama cha Karate kilichoshiriki Mashindano ya Afrika Mashariki jijini Nairobi nchini Kenya pamoja na Timu ya Taifa ya Wanawake ya Kabaddi iliyoshiriki Mashindano ya Dunia ya mchezo huo yaliyofanyika nchini Bangladesh.

71. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, Zanzibar imefanikiwa kuratibu na kuwa mwenyeji wa Mashindano ya CHAN 2024 kwa mafanikio makubwa tukishirikiana na nchi za Kenya, Uganda na Tanzania Bara. Aidha, Wizara imefanikiwa kuandaa mashindano ya NMB Mapinduzi Cup 2026 kwa udhamini wa wadau mbalimbali wakiwemo Benki ya NMB, Azam Media, Benki ya PBZ na washirika wengine. Hatua hii imeongeza ushiriki wa kimataifa na kukuza utalii wa michezo Zanzibar.

### C.5.2 Changamoto

72. **Mheshimiwa Spika,** mbali na mafanikio hayo, Wizara imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Miongoni mwa changamoto hizo ni Wakala wa Serikali wa Uchapaji kushindwa kununua malighafi moja kwa moja kutoka viwandani kutokana na ufinyu wa mtaji pamoja na masharti ya kisheria yanayotolewa na Mamlaka ya ununuzi yanayozuia ununuzi wa malighafi unaozidi shilingi bilioni 5. Aidha, kuna changamoto ya ongezeko la madeni yanayodaiwa na Wakala wa Serikali wa Uchapaji pamoja na Shirika la Magazeti ya Serikali kutoka kwa taasisi zilizopatiwa huduma, hali inayodhoofisha ufanisi wa utoaji wa huduma hizo. Vilevile, Shirika la Magazeti linakabiliwa na gharama kubwa za uchapishaji kutokana na kukosekana kwa mtambo wa uchapishaji wa ndani, hivyo kulazimika kutumia huduma za kampuni binafsi.

73. **Mheshimiwa Spika,** changamoto nyengine ni kutopatikana au kuchelewa kwa huduma za baadhi ya mifumo shirikishi ya Serikali kama ePROZ, ZanMalipo, eOffice na ZanKibali kutokana na changamoto za kimtandao kunapelekea kuchelewesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara, kupungua kwa ufanisi wa utoaji wa huduma, na usumbufu kwa watumishi pamoja na wananchi; kuongezeka kwa ushindani wa utoaji wa huduma katika sekta ya habari kumeathiri upatikanaji wa matangazo kwa Shirika la Utangazaji na Shirika la Magazeti. Aidha, Kukosekana kwa ofisi za kudumu za ZBC na Shirika la Magazeti kwa upande wa Tanzania Bara imekuwa changamoto na hivyo kusababisha matumizi ya ofisi ndogo za uratibu, jambo ambalo limeathiri ufanisi wa utekelezaji wa majukumu, upatikanaji wa huduma kwa wakati na uratibu mzuri wa shughuli za taasisi hizo.

74. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuongezea, Wizara inakabiliwa na changamoto mbalimbali katika sekta ya michezo ikiwemo upungufu wa wataalamu wa fani tofauti za michezo kama makocha, waamuzi,

waandaaji wa mashindano na wataalamu wa tiba ya michezo, jambo ambalo linaathiri uendelezaji na uboreshaji wa vipaji vya wanamichezo. Aidha, kuna changamoto ya ukosefu wa wadhamini wa kutosha katika sekta ya michezo, hali inayosababisha kushindwa kufadhili kikamilifu mashindano, programu za maendeleo ya michezo na ujenzi wa miundombinu ya michezo. Vilevile, kuna kufifia kwa baadhi ya michezo kama mpira wa vinyoya, mpira wa meza, mpira wa magongo na kutunisha misuli kutokana na ukosefu wa miundombinu rafiki, vifaa vya kisasa na programu endelevu za kuibua na kukuza vipaji vya michezo hiyo.

75. **Mheshimiwa Spika,** sio hayo tu lakini pia, Wizara kama msimamizi mkuu wa masuala ya utamaduni Zanzibar, inakabiliwa na changamoto ya mmong'onyoko wa maadili ya Kizanzibari unaochangiwa kwa kiasi kikubwa na athari za utandawazi, hususan kupitia mitandao ya kijamii na mabadiliko ya kasi ya teknolojia ya habari na mawasiliano, hali inayosababisha kuongezeka kwa tabia na mienendo isiyoendana na mila, desturi na utamaduni wa jamii ya Kizanzibari. Aidha, kuna changamoto ya ukosefu wa miundombinu ya kisasa ya sanaa kama kumbi za maonesho, vituo vya mafunzo ya sanaa na vifaa stahiki vya kisanii, pamoja na upungufu wa wataalamu wabobezi katika fani mbalimbali za sanaa, hali inayokwamisha ukuaji na ubunifu katika sekta hiyo. Vilevile, kwa upande wa lugha yetu ya Kiswahili inakabiliwa na changamoto za upungufu wa wataalamu wa lugha hususan katika tafsiri na ukalimani, matumizi yanayoendelea kuongezeka ya lugha mchanganyiko na isiyo sanifu kutokana na ushawishi wa mitandao ya kijamii, pamoja na athari za lugha za kigeni zinazoathiri ufasaha na usanifu wa Kiswahili fasaha.

## D. MUELEKEO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI KWA KILA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

76. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji kwa kila programu zinazosimamiwa na Wizara ya Habari, Sanaa,

Utamaduni na Michezo kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2025/2026, kwa ruhsa yako sasa, naomba kuwasilisha muelekeo wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

### 1.1. IPAUMBELE VIKUU VYA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

77. **Mheshimiwa Spika,** matayarisho ya bajeti hii yamezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (2050), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2025-2030), Sera ya Habari (2023), Sera ya Michezo (2018), Sera za Sekta Mtambuka za Taifa, Mpango Mkakati wa Wizara na Taasisi zake, Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya ufunguzi wa Baraza la 11 la Wawakilishi, Ahadi na Maagizo mbalimbali yaliyotolewa na Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

78. **Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia miongozo hiyo, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027, Vipaumbele vikuu vya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ni:- Kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa habari; Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa vyombo vya habari, uchapaji na utangazaji; Kutoa elimu kwa jamii juu ya kulinda mila, silka na utamaduni wa mzanzibari; Kusimamia shughuli za Sanaa na Burudani; Kuendeleza, kukuza na kueneza matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu; Kusimamia na kuimarisha miundombinu ya michezo; Kuratibu maendeleo ya michezo nchini; Kusimamia matayarisho na uratibu wa mashindano ya AFCON 2027; kutayarisha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali itakayowezesha kusimamia pamoja na kutoa huduma bora kwa jamii katika sekta za Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

### D.2. MUHTASARI WA MAELEZO KWA KILA PROGRAMU NA MALENGO YANAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

79. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo imepanga kutekeleza

Programu Kuu 3 kama ifuatavyo: i) Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji; ii) Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na iii) Programu ya Uendeshaji na Mipango katika sekta za Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Programu hizo zitatekelezwa katika Fungu 056, ambapo Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji itatekelezwa pia katika Fungu 107.

80. **Mheshimiwa Spika,** programu kuu zilizoainishwa katika bajeti hii zimewekewa malengo makhususi, matokeo ya muda mrefu yatakayopatikana, huduma zitakazotolewa, shabaha na viashiria mbalimbali vitakavyotumika kupima utekelezaji wa huduma zitakazotolewa katika sekta za Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo. Maelezo ya programu hizo ni kama ifuatavyo:

## FUNGU 056 WIZARA YA HABARI SANAA UTAMADUNI NA MICHEZO

### D.2.1. PROGRAMU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

81. **Mheshimiwa Spika,** matokeo ya programu hii ni kuimarika kwa mfumo jumuishi wa habari, utangazaji na uchapaji utakaowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi, kuongeza ubora wa maudhui na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji itakuwa na Programu ndogo mbili ambazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji.

#### D.2.1.1. Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari

82. **Mheshimiwa Spika,** programu hii ndogo inasimamiwa na Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) na Shirika

la Magazeti ya Serikali (SMS). Programu ndogo hii ina lengo la kuhakikisha upatikanaji na usambazaji wa habari sahihi, kwa wakati na kwa uwazi kwa wananchi wote ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya jamii. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara kupitia Idara na Taasisi zinazosimamia programu hii, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

**IDARA YA HABARI MAELEZO**

**83. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Habari Maelezo kupitia programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukusanya na kusambaza taarifa za Serikali kwa vyombo vya habari na umma, picha, matangazo na Makala;
ii. Kuandaa mikutano ya Mawaziri, Wakuu wa Taasisi za SMZ na vyombo vya Habari;
iii. Kufanya mikutano ya maafisa habari wa SMZ na kutoa tunzo kwa waandishi wa habari; na
iv. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

**84. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Habari Maelezo imepanga kutumia jumla ya **TZS 1,041,572,210/-** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **TZS 641,572,210/-** ni mishahara na **TZS 400,000,000/-**ni matumizi ya uendeshaji. Vile vile, Idara ya Habari Maelezo inakadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 93,500,000/-**

**SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)**

**85. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Shirika la Utangazaji Zanzibar kupitia programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuandaa na kurusha habari, vipindi, matangazo pamoja na matukio mbali mbali kupitia Televisheni, Redio na mitandao ya kijamii;
ii. Kusimamia na kufuatilia shughuli za masoko na uwekezaji;
iii. Kusimamia na kufuatilia shughuli za uunganishaji na usambazaji wa maudhui;
iv. Kusimamia vituo vya Shirika la Utangazaji Pemba, Dar- es- Salaam na Dodoma; na
v. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

**86. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Shirika la Utangazaji Zanzibar limepanga kutumia jumla ya **TZS 3,495,180,000/-** kwa ajili ya mishahara.

## SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI (SMS)

**87. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Shirika la Magazeti ya Serikali kupitia programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuimarisha shughuli za uchapishaji na usambazaji wa magazeti;
ii. Kulitangaza Shirika ili kuendana na mabadiliko ya biashara na mahitaji ya soko;
iii. Kutengeneza na kuimarisha mifumo ya TEHAMA;
iv. Kuimarisha huduma za gazeti mtandao;
v. Kuandaa vikao vya Bodi ya wakurugenzi na Bodi ya Zabuni;na
vi. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

**88. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Shirika la Magazeti ya Serikali imepanga kutumia jumla ya **TZS 1,260,381,000/-** kwa ajili ya mishahara.

### D.2.1.2. Programu ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji

89. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inasimamiwa na Idara ya Habari Maelezo na Wakala wa Serikali wa Uchapaji. Programu hii ina lengo la Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa vyombo vya habari, utangazaji na uchapaji ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, maadili na utoaji wa maudhui yenye ubora kwa manufaa ya jamii. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara kupitia Taasisi zinazosimamia programu hii, imepanga kutekeleza malengo yafuatayo: -

**IDARA YA HABARI MAELEZO**

90. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Habari Maelezo kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa vitambulisho vya waandishi wa habari;
ii. Kusajili magazeti na majarida na Mawakala wa habari;
iii. Kutoa vibali vya upigaji wa picha kwenye maeneo ya mji wa Zanzibar; na
iv. Kufanya vikao vya Bodi.

91. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Habari Maelezo imepanga kutumia jumla ya **TZS 70,500,000/-** Kwa matumizi ya uendeshaji.

**WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR**

92. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wakala wa Serikali wa Uchapaji kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kusimamia shughuli za uchapaji;
ii. Kuwapatia vifaa vya kisasa vya uchapaji na kusimamia mifumo ya TEHAMA;
iii. Kukuza na kuimarisha masoko ili kupanua wigo wa wateja;
iv. Kuimarisha shughuli za bohari kuu ya vifaa vya kuandikia; na
v. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

**93. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wakala wa Serikali wa Uchapaji imepanga kutumia jumla ya **TZS 2,213,260,000/-** kwa ajili ya mishahara.

### D.2.2. PROGRAMU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

**94. Mheshimiwa Spika,** matokeo ya programu hii ni kuimarika kwa uhifadhi na ukuzaji wa utamaduni, kuimarika kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili sanifu na fasaha, kuongezeka kwa ubunifu na ushindani wa sanaa pamoja na maendeleo ya michezo yatakayochochea ajira, uchumi na utambulisho wa taifa. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu kuu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo itakuwa na Programu ndogo mbili ambazo ni program ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi, Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa; na Programu ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Michezo.

#### D.2.2.1 Programu ndogo ya Uimarishaji,Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa

**95. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inasimamiwa na Idara ya Utamaduni; Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu (BASSFU); na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA). Programu hii ina lengo la kuimarisha, kuhifadhi na kuendeleza utamaduni na sanaa kwa kukuza ubunifu, kulinda urithi wa taifa na kuimarisha matumizi ya Kiswahili kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka wa

fedha 2026/2027, Wizara kupitia Idara na Taasisi zinazosimamia programu ndogo hii, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

## IDARA YA UTAMADUNI

96. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Utamaduni kupitia programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuandaa Tamasha la Utamaduni wa Mzanzibari na kuyaendeleza Matamasha ya kijamii Unguja na Pemba;
ii. Kukuza, kuhifadhi na kutangaza utamaduni wa jamii ya Zanzibar kupitia vyombo vya habari;
iii. Kujenga Kijiji cha Utamaduni Zanzibar;
iv. Kuviwezesha vikundi vya sanaa, wasanii, pamoja na wajasiriamali wa bidhaa za kiutamaduni kushiriki katika matamasha ya Kitaifa na Kimataifa;
v. Kutoa elimu ya kulinda, kuhifadhi na kuendeleza mila, silka na desturi za Mzanzibari; na
vi. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

97. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Utamaduni imepanga kutumia jumla ya **TZS 17,881,834,570/-** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS 2,881,834,570/-** (**TZS 2,371,876,570/-** ni mishahara na **TZS 509,958,000/-** za uendeshaji) na **TZS 15,000,000,000/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## BARAZA LA SANAA NA SENSA YA FILAMU (BASSFU)

98. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu (BASSFU) kupitia programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kukagua maeneo na taasisi zinazojishuhulisha na burudani;
ii. Kuibua vipaji vya Sanaa kwa wanafunzi wa skuli za msingi;
iii. Kuandaa mafunzo ya wasanii na wadau wa Sanaa;
iv. Kuimarisha shirikisho la Sanaa na vyama vya Sanaa;
v. Kuendelea na ukaguzi wa Filamu na kazi za Sanaa za maonyesho;
vi. Kuendelea kuwajengea uwezo wasanii kwa kuwapatia mafunzo na utaalamu; na
vii. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

**99. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu (BASSFU) imepanga kutumia jumla ya **TZS 829,250,000/-** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji. Vile vile, Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu (BASSFU) linakadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 370,000,000/-**

## BARAZA LA KISWAHILI ZANZIBAR (BAKIZA)

**100. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) kupitia programu ndogo ya Uimarishaji, Uhifadhi na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuhamasisha na kuendeleza utumiaji sahihi wa Lugha ya Kiswahili ndani na nje, kwa kupitia mafunzo mbalimbali, makongamano, matamasha na mikutano ya Kimataifa ya Kiswahili;
ii. Kufanya maadhimisho ya siku ya Kiswahili duniani pamoja na kuandaa kongamano la 10 la Kiswahili la kimataifa;
iii. Kutoa mafunzo ya kiswahili kwa wageni na wataalamu
iv. Kusambaza machapisho na vitabu;
v. Kuandaa programu za kubadilishana uzoefu;
vi. Kufanya uhariri wa vitabu, Makala na kazi za uandishi; na
vii. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

101. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) limepanga kutumia jumla ya **TZS 700,340,000/-** kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji. Vile vile, Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) linakadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 41,500,000/-**

### D.2.2.2 Programu ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo

102. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inasimamiwa na Idara ya Michezo na Baraza la Taifa la Michezo (BTMZ). Programu hii ina lengo la kukuza na kuendeleza shughuli za michezo kwa kuimarisha miundombinu, vipaji na ushiriki wa jamii ili kuongeza ushindani, afya na ajira. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara kupitia Idara na Taasisi zinazosimamia programu ndogo hii, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

## IDARA YA MICHEZO ZANZIBAR

103. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Michezo kupitia programu ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kujenga na kuimarisha viwanja vya michezo Zanzibar;
ii. Kuwezesha timu za Taifa kushiriki katika mashindano ya Kikanda na Kimataifa;
iii. Kusaidia kuandaa mashindano ya Kimataifa;
iv. Kuandaa mashindano ya mawizara, mashirika na taasisi za serikali;
v. Kuwawezesha Maafisa wa Idara, viongozi wa vyama vya michezo, waamuzi na makocha kushiriki mafunzo ya Kimataifa
vi. Kuandaa bonanza la mazoezi Kitaifa;
vii. Kuratibu mikutano ya wadau wa michezo ; na
viii. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

**104. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Michezo imepanga kutumia jumla ya **TZS 205,262,320,000/-** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya na **TZS 360,000,000/-** ni matumizi ya uendeshaji na **TZS 204,902,320,000/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

## BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO (BTMZ)

**105. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ) kupitia programu ndogo ya Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuhamasisha jamii kushiriki katika michezo kwa kuandaa mashindano ya ndani na kitaifa;
ii. Kuviwezesha vyama vya michezo vya watu wenye ulemavu kushiriki katika michezo;
iii. Kuandaa mkutano mkuu wa wadau wa Michezo;
iv. Kuimarisha Mabaraza ya michezo ya Wilaya;
v. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi; na
vi. Kuratibu mashindano ya Kimataifa ya AFCON 2027.

**106. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Baraza la Taifa la Michezo limepanga kutumia jumla ya **TZS 5,695,810,000/-** Kati ya fedha hizo **TZS 695,810,000/-** kwa ajili ya kazi za kawaida na **TZS 5,000,000,000/-** kwa ajili ya uratibu wa Mashindano ya AFCON 2027. Vile vile, Baraza la Taifa la Michezo linakadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 6,500,000/-**

## D.2.3. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO

**107. Mheshimiwa Spika,** matokeo ya programu hii ni kuimarika kwa uratibu, usimamizi na upangaji wa shughuli za sekta ya habari,

sanaa, utamaduni na michezo kwa ufanisi, uwazi na tija, hivyo kuongeza ubora wa huduma na kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo itakuwa na Programu ndogo tatu ambazo ni Programu ndogo ya Uratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara; Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji na Programu ndogo ya Uratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

### D.2.3.1. Programu Ndogo ya Uratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara

108. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Programu hii ina lengo la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango mikuu ya wizara kwa ufanisi ili kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali na kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara kupitia Idara inayosimamia programu ndogo hii, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanya tathmini na maandalizi ya sera, sheria na kanuni za Wizara;
ii. Kusimamia na kuratibu mipango ya Wizara;
iii. Kufanya ufuatiliaji wa miradi na programu za Wizara;
iv. Kufanya tafiti katika sekta za habari, sanaa, utamaduni na michezo;
v. Kukusanya na kuhifadhi takwimu za utekelezaji kwa Wizara na taasisi zake na kuandaa kanzi data;
vi. Kuratibu na kushiriki vikao vya ushirikiano kati ya SMZ na SMT na vikao vya kikanda na kimataifa; na
vii. Kuratibu vikao vya wadau na Kazi za Kamati za BLW.

109. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imepanga kutumia jumla ya **TZS 338,812,220/-** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

### D.2.3.2. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

**110. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inasimamiwa na Idara ya Utawala na Uendeshaji. Programu hii ina lengo la kuimarisha utawala na uendeshaji wa wizara kwa kuhakikisha matumizi bora ya rasilimali, uwajibikaji na utoaji wa huduma kwa ufanisi. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara kupitia Idara inayosimamia programu ndogo hii, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kutekeleza Sheria ya manunuzi na Sheria ya fedha ya Wizara
ii. Kushiriki mikutano na ziara mbalimbali za kitaifa, kikanda na kimataifa;
iii. Kutekeleza shughuli za Wizara na shughuli za wadau za Wizara;
iv. Kuimarisha kitengo cha Habari na Mawasiliano cha Wizara;
v. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

**111. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Idara ya Utawala na Uendeshaji imepanga kutumia jumla ya **TZS 2,984,688,000/-** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na mishahara. Kati ya fedha hizo **TZS 1,775,188,000/-** ni mishahara na **TZS 1,209,500,000/-** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji.

### D.2.3.3. Programu Ndogo ya Uratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

**112. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii inasimamiwa na Ofisi Kuu Pemba. Programu hii ina lengo la Kuratibu na kusimamia shughuli za utawala, uendeshaji na mipango ya Ofisi Kuu Pemba kwa ufanisi ili kuhakikisha utoaji bora wa huduma na utekelezaji wa majukumu ya wizara. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara kupitia Ofisi Kuu Pemba inayosimamia programu ndogo hii, imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuratibu shughuli za utafiti Pemba;
ii. Kuratibu shughuli za sera;
iii. Kuratibu ziara na vikao vya kamati za Baraza La Wawakilishi;
iv. Kuweka kumbukumbu zinazohusu Programu, Miradi na shughuli nyengine za Wizara kwa upande wa Pemba;
v. Kuandaa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya kanuni za Utumishi pamoja na masuala mtambuka;
vi. Kuratibu na kutekeleza shughuli za wadau wa Wizara;
vii. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya miradi na shughuli za Wizara Pemba; na
viii. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

113. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Ofisi Kuu Pemba imepanga kutumia jumla ya **TZS 1,578,792,000/**- kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Kawaida. Kati ya fedha hizo **TZS 1,148,792,000/-** ni mishahara na **TZS 430,000,000/-** ni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji. Vile vile, Ofisi Kuu Pemba inakadiriwa kukusanya jumla ya **TZS 70,000,000/-**

## FUNGU 107: TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR

## D.3 PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI NA UTANGAZAJI

114. **Mheshimiwa Spika,** matokeo yanayotarajiwa katika programu hii kupitia Fungu J05 ni kuimarika kwa usimamizi na udhibiti wa sekta ya utangazaji ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora, maudhui yenye kuzingatia maadili, na ulinzi wa maslahi ya umma. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji itakuwa na Programu ndogo mbili ambazo ni Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji na Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji.

### D.3.1 Programu Ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji

**115. Mheshimiwa Spika,** programu ndogo hii ina lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa sekta ya utangazaji ili kuhakikisha uzingatiaji wa sheria, kanuni na maadili ya taaluma. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Tume ya Utangazaji Zanzibar kupitia programu ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya habari, Utangazaji na Uchapaji imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanya ukaguzi na ufuatiliaji wa maudhui ya vituo vya utangazaji;
ii. Kuandaa kanuni na miongozo ya huduma za utangazaji;

**116. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, katika programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji Tume ya Utangazaji Zanzibar imepanga kutumia jumla ya **TZS 331,155,000/-**kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji.

### D.3.2 Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji

**117. Mheshimiwa Spika,** lengo la programu hii ni kuimarisha ufanisi wa kiutawala na usimamizi wa rasilimali watu, fedha na vifaa ili kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa ufanisi. Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Tume ya Utangazaji Zanzibar kupitia programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa elimu kwa watendaji wa vituo vya utangazaji juu ya matumizi ya teknolojia mpya katika utangazaji na namna ya utayarishaji wa maudhui bora;
ii. Kuandaa kongamano la vituo vya utangazaji ili kuimarisha mashikiriano katika usimamizi wa sekta ya utangazaji; na
iii. Kuweka mazingira bora ya kazi, kulipa stahiki na kuwajengea uwezo wafanyakazi.

118. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Tume ya Utangazaji Zanzibar kupitia programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji imepanga kutumia jumla ya **TZS 1,233,725,000/-** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na mshahara, Kati ya fedha hizo **TZS 749,660,000/**- ni mishahara na **TZS 484,065,000/-** ni matumizi ya uendeshaji.

## F: MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 FUNGU 056

119. **Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuiwezesha Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kutekeleza Programu Kuu tatu (3) zilizomo katika Fungu 056, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu liridhie makadirio ya matumizi yenye jumla ya **TZS 243,352,740,000/-** kati ya fedha hizo, **TZS 23,450,420,000/-** ni kwa ajili ya kazi za kawaida (**TZS 12,906,249,780/-** ni mishahara, **TZS 10,544,170,220/-**ni matumizi ya uendeshaji) na **TZS 219,902,320,000/-** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. **Kiambatanisho nambari 1F na 1G kinahusika.**

120. **Mheshimiwa Spika,** vile vile naliomba Baraza lako kuidhinisha ukusanyaji wa mapato yenye jumla ya **TZS 581,500,000/-** ikiwa ni makusanyo yanayoingia mfuko mkuu wa Serikali. Kiambatanisho nambari 1H kinahusika

## FUNGU 107 TUME YA UTANGAZAJI ZANZIBAR

121. **Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha Tume ya Utangazaji Zanzibar kutekeleza kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya programu zenye jumla ya **TZS 1,564,880,000/-** kwa matumizi ya kazi za kawaida. (**TZS 749,660,000/-** ni mishahara, **TZS 815,220,000/-**ni matumizi ya uendeshaji). kiambatisho nambari 1F na 1G kinahusika

122. **Mheshimiwa Spika,** vile vile naliomba Baraza lako kuidhinisha ukusanyaji wa mapato yenye jumla ya **TZS 400,000,000/-** ikiwa

ni makusanyo yanayoingia mfuko mkuu wa Serikali. Kiambatanisho nambari 1H kinahusika

## G. SHUKURANI

**123.** **Mheshimiwa Spika**, kabla sijamaliza hotuba yangu hii sina budi kutoa shukran zangu za dhati kwako na kwa waheshimiwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa miongozo, maoni na ushauri mnayoendelea kutupatia kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Wizara yetu.

**124.** **Mheshimiwa Spika,** pia naomba nichukuwe fursa hii kwa mara nyengine tena kumshukuru sana **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduz**i kwa ujasiri wake wa kuiletea maendeleo Zanzibar. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema yeye na familia yake ili aendelee kutuongoza kwa mafanikio makubwa.

**125.** **Mheshimiwa Spika,** shukran za dhati ziende kwa Chama changu cha Mapinduzi kuanzia ngazi ya shina hadi Taifa. Ninakishukuru Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Kaskazini Unguja sambamba na Jumuiya ya Wanawake (U.W.T) ngazi ya matawi hadi Taifa, U.W.T Mkoa wa Kaskazini Unguja na nawashukuru kwa dhati kwas mapenzi, umoja na mshikamano wao katika kuhakikisha malengo ya Chama chetu cha Mapinduzi yanafanikiwa.

**126.** **Mheshimiwa Spika,** shukran pia ziwaendee viongozi wastaafu wa Wizara ambao walifanya kazi kubwa ya kuhakikisha mipango yote ya Wizara ya Habari inafanikiwa ipasavyo, kipekee shukrani hizo ziende kwa Mheshimiwa Tabia Maulid Mwita aliekuwa Waziri wa Habari, Vijana, utamaduni na Michezo na Ndugu Fatma Hamadi Rajab aliekuwa Katibu Mkuu. Tunawashukuru sana kwa jitihada zao kubwa walizozichukua kuhakikisha Wizara hii inasonga mbele.

**127.** **Mheshimiwa Spika,** mafanikio ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo ambayo nimeyaeleza kwa kina katika hotuba

hii, ni matokeo ya ushirikiano wa wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi. Kwa niaba ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo napenda kuchukuwa fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza Taasisi mbalimbali tunazoshirikiana nazo katika kuendeleza Sekta zilizo chini ya Wizara hii. Shukran za dhati ziende kwa mashirikisho na vyama mbalimbali vya michezo, wasanii, Benki ya NMB, Azam Media na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), CRDB Bank, Azania Bank, Zanzibar School of Health (ZSH), ZSSF, ZURA, TAMWA, NSSF, ZRA, ZBC, IRIS, TRA, ZIC, NSSSF, ZURA, Orkun Group Company, Reform Sports, Hoteli ya Golden Tulip ya Airport Zanzibar na Hoteli ya Madinatul Bahar.

128. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, natoa shukrani zangu za dhati kwa Taasisi na majukwaa yanayotoa huduma za kihabari zikiwemo Jukwaa la Wahariri, Baraza la Habari, Asasi za Kiraia zinazosaidia wasanii pamoja na Washirika wote wa Maendeleo tulioshirikiana nao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, Shukrani kwa wanahabari wote na wadau wa Habari wote, wasanii wote na wanasanaa, wadau wote wa utamaduni, wanamichezo na wadau wa michezo. Taasisi na majukwaa haya yamechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha Sekta za Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo hapa Zanzibar. Kwa niaba ya Serikali na kwa kupitia Baraza lako naomba kutoa wito, kuwaomba wadau waliotajwa hapo juu na wengineo kuendelea kushirikiana na Serikali katika kutoa huduma za Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo.

129. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati viongozi wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo nikianzia na Mheshimiwa Ali Abdul-ghulam Hussein, Naibu Waziri wa Habari ambae pia ni Muwakilishi wa Jimbo la Jan'gombe, Ndg. Mattar Zahor Masoud, Katibu Mkuu, Ndg. Makame Machano Haji, Naibu Katibu Mkuu na Ndg. Mfamau Lali Mfamau, Afisa Mdhamini Wizara ya Habari. Naomba pia nitoe shukrani zangu za kipekee kwa Wakurugenzi wote, Makamishna, Makatibu Watendaji, Maafisa

Mipango na wafanyakazi wote wa Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo Unguja na Pemba, kutokana na juhudi zao kubwa, ushirikiano mzuri na kujituma kwa dhati katika kutekeleza majukumu yao na kufanikisha malengo ya Wizara.

130. **Mheshimiwa Spika,** ni matumaini yangu kwamba maelezo niliyoyatoa katika hotuba hii ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo yanatosha katika kuliarifu Baraza lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai hadi Machi, 2025/2026 na mpango wa utekelezaji wa majukumu kwa kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2026/2027, hivyo ni matumaini yangu kwamba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako wataichangia hotuba hii ipasavyo.

131. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa nawaomba wajumbe wa Baraza lako waipokee, waijadili, watushauri, watuelekeze na baadae watupitishie Bajeti ya Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

132. **Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa hoja.



**Dkt. Riziki Pembe Juma (MBM)**
**Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo**
**Zanzibar.**

## VIAMBATANISHO

| *KIAMBATISHO NAMBA 1 A* | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **FEDHA ZILIZOINGIZWA KUANZIA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 KWA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU** | | | | | |
| **NO** | **IDARA** | **MAELEZO** | **BAJETI 205/2026** | **FEDHA ZILIZOPATIKANA JULY -MARCH 2025/2026** | **ASILIMIA** |
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 976,614,000 | 716,568,848 | 73% |
| | | Matumizi Mengineo | 400,000,000 | 273,877,850 | 68% |
| | **JUMLA** | | **1,376,614,000** | **990,446,698** | **72%** |
| 2 | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 315,800,000 | 110,000,000 | 35% |
| | **JUMLA** | | **315,800,000** | **110,000,000** | **29%** |
| 3 | Uendeshaji na Utumishi | Mishahara | 1,357,168,000 | 1,198,462,638 | 88% |
| | | Matumizi Mengineo | 1,080,000,000 | 596,697,178 | 55% |
| | **JUMLA** | | **2,437,168,000** | **1,795,159,816** | **74%** |
| 4 | Maendeleo ya Vijana | Mishahara | 594,592,000 | 385,515,567 | 65% |
| | | Matumizi Mengineo | 722,610,690 | 137,185,000 | 19% |
| | **JUMLA** | | **1,317,202,690** | **522,700,567** | **40%** |
| 5 | Idara ya Utamaduni | Mishahara | 2,448,234,000 | 1,757,428,364 | 72% |
| | | Matumizi Mengineo | 403,025,000 | 155,000,000 | 38% |
| | **JUMLA** | | **2,851,259,000** | **1,912,428,364** | **67%** |
| 6 | Idara ya Michezo | Mishahara | - | - | - |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Matumizi Mengineo | 497,714,967 | 296,790,000 | 60% |
| | **JUMLA** | | **497,714,967** | **296,790,000** | **60%** |
| 7 | Idara ya Habari Maelezo | Mishahara | 778,392,000 | 416,930,713 | 54% |
| | | Matumizi Mengineo | 485,810,033 | 109,000,000 | 22% |
| | **JUMLA** | | **1,264,202,033** | **525,930,413** | **42%** |
| | **Jumla ya Mishahara** | | **6,155,000,000** | **4,474,906,128** | **73%** |
| | **Jumla ya Matumizi Mengine** | | **3,908,511,000** | **1,678,550,028** | **43%** |
| | **Jumla Kuu kwa Taasisi zisizopokea Ruzuku** | | **10,063,511,000** | **6,153,456,156** | **61%** |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | **TAASISI ZA RUZUKU** | | | | |
| | | | | | |
| 1 | Baraza la Vijana Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 443,300,000 | 268,728,024 | 61% |
| | | | **443,300,000** | **268,728,024** | **61%** |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | | | - |
| | | Matumizi Mengineo | 353,100,000 | 165,852,173 | 50% |
| | **JUMLA** | | **353,100,000** | **165,852,173** | **50%** |
| 4 | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu na Utamaduni Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 691,000,000 | 175,459,321 | 25% |
| | **JUMLA** | | **691,000,000** | **175,459,321** | **25%** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | - | - | - |
| | | Matumizi Mengineo | 350,500,000 | 105,437,811 | 30% |
| | **JUMLA** | | **350,500,000** | **105,437,811** | **30%** |
| 6 | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 777,500,000 | 555,974,700 | 72% |
| | | Matumizi Mengineo | 679,400,000 | 217,505,858 | 32% |
| | **JUMLA** | | **1,456,900,000** | **773,480,558** | **53%** |
| 7 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 3,842,900,000 | 2,505,010,870 | 65% |
| | | Matumizi Mengineo | - | - | |
| | **JUMLA** | | **3,842,900,000** | **2,505,010,870** | **65%** |
| 8 | Shirika la Magazeti | Mishahara | 1,587,500,000 | 931,345,459 | 59% |
| | | Matumizi Mengineo | - | - | |
| | **JUMLA** | | **1,587,500,000** | **931,345,459** | **59%** |
| 9 | kampuni ya Uunganisha Maudhui | Mishahara | | | - |
| | | Matumizi Mengineo | | | |
| | **JUMLA** | | | | |
| 10 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji (ZGP) | Mishahara | 2,475,300,000 | 1,621,372,434 | 66% |
| | | Matumizi Mengineo | - | - | - |
| | **JUMLA** | | **2,475,300,000** | **1,621,372,434** | **66%** |
| | **Jumla y Mishahara y Ruzuku** | | **8,683,200,000** | **5,613,703,462** | **65%** |
| | **Jumla ya matumizi ya Ruzuku** | | **2,517,300,000** | **732,983,186** | **29%** |
| | **JUMLA KUU** | | **11,200,500,000** | **6,346,686,648** | **51%** |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **YA RUZUKU** | | | | |
| | **Jumla ya Mishahara kwa Wizara** | | **6,155,000,000** | **4,474,906,128** | **73%** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara** | | **3,908,511,000** | **1,678,550,028** | **43%** |
| | **JUMLA YA WIZARA** | | **10,063,511,000** | **6,153,456,156** | **61%** |
| | **JUMLA YA MISHAHARA KWA WIZARA** | | **14,838,200,000** | **10,088,609,590** | **68%** |
| | **JUMLA YA MATUMIZI MENGINEYO YA WIZARA** | | **6,425,811,000** | **2,411,533,214** | **38%** |
| | **JUMLA KUU Y WIZARA MATUMIZI Y KAWAIDA (A)** | | **21,264,011,000** | **12,500,442,804** | **59%** |
| | **Miradi ya Maendeleo** | | | | |
| 1 | Uimarishaji wa Michezo na miundombinu ya viwanja vya michezo. | | 389,400,000,000 | 154,242,490,091 | 40% |
| 2 | Ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Mikoa | | 40,550,000,000 | 38,304,822,647 | 94% |
| 3 | Ujenzi wa wa viwanja vya michezo midogo midogo - GIZ | | 633,982,000 | - | 0% |
| 4 | Ujenzi wa vituo vya maendeleo ya vijana | | 16,500,000,000 | 2,227,613,300 | 14% |
| 5 | Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa | | 3,000,000,000 | 1,953,025,138 | 65% |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6 | Uendeshaji wa mashindano ya CHAN | - | 2,734,845,120 | 100% |
| | **Jumla Kuu ya Wizara Miradi ya Maendeleo (B)** | **433,583,982,000** | **199,462,796,296** | 46**%** |
| | **JUMLA KUU A WIZARA (A+B)** | **454,847,993,000** | **211,962,939,100** | **47%** |

***KIAMBATISHO NAMBA 1B***

***MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI MACHI 2026***

**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| NO | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu | 360,000,000 | 279,524,000 | 78% |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 50,000,000 | 10,933,500 | 22% |
| 3 | Habari Maelezo | 200,000,000 | 13,274,750 | 7% |
| 4 | Ofisi kuu Pemba | 100,000,000 | 14,705,000 | 15% |
| | **JUMLA** | **710,000,000** | **318,437,250** | **45%** |

***MAPATO YANAYOTUMIWA NA TAASISI HUSIKA***

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | MAPATO YALIYOKUSANYWA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 3,300,000,000 | 2,219,100,259 | 67% |
| 2 | Shirika la Magazeti (SMS) | 1,500,000,000 | 860,132,581 | 57% |
| 3 | ZGP | 3,607,952,000 | 4,853,371,078 | 135% |
| 5 | Tume ya Utangazaji | 320,000,000 | 139,600,000 | 44% |
| | **JUMLA** | **8,727,952,000** | **8,311,663,057** | **95%** |

*KIAMBATISHO NAMBA 1D*

***FEDHA ILIYOPATIKANAJULAI 2025 HADI MACHI 2026 KWA KILA PROGRAMUNDOGO***

**Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa habari**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Habari Maelezo | 188,290,000 | 83,830,000 | 45% |
| 2 | Shirika la Utangazaji ZBC | 3,842,900,000 | 2,505,010,870 | 65% |
| 3 | Shirika la Magazeti ya Serikali | 1,587,500,000 | 931,345,459 | 59% |
| | **JUMLA** | **5,618,690,000** | **3,520,186,329** | **63%** |

**Programu ndogo ya Usimamizi wa Vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapishaji**

| NO | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| | Idara ya habari Maelezo | 1,075,912,033 | 442,100,413 | 41% |
| | Tume ya Utangazaji | 1,456,900,000 | 773,480,558 | 53% |
| | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 2,475,300,000 | 1,621,372,434 | 66% |
| | **JUMLA** | **5,008,112,033** | **2,836,953,405** | **57%** |

**Programu Ndogo ya Maendeleo ya Vijana**

| NO | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Maendeleo ya Vijana | 1,317,202,690 | 522,700,567 | 40% |
| 2 | Baraza la Vijana | 443,300,000 | 268,728,024 | 61% |
| 3 | Ujenzi wa Vituo vya Maendeleo Vijana | 16,500,000,000 | 2,227,613,300 | 14% |
| | **Jumla** | **18,260,502,690** | **3,019,041,891** | **17%** |

**Programu ndogo ya Uimarishaji na Uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utamaduni | 2,851,259,000 | 1,912,428,364 | 67% |
| 2 | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu | 691,000,000 | 175,459,321 | 25% |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 353,100,000 | 165,852,173 | 50% |
| 4 | Ujenzi wa Nyumba ya Sanaa | 3,000,000,000 | 1,953,025,138 | 65% |
| | **JUMLA** | **6,895,359,000** | **4,206,764,996** | **61%** |

**Programu ndogo ya Uendelezaji na Ukuzaji wa Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Michezo | 497,714,967 | 296,790,000 | 60% |
| 2 | Baraza la Taifa la Michezo | 350,500,000 | 105,437,811 | 30% |
| 3 | Uimarishaji wa Michezo na miundombinu ya viwanja vya michezo. | 372,900,000,000 | 154,242,490,091 | 40% |
| 4 | Ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Mikoa | 40,550,000,000 | 38,304,822,647 | 94% |
| 5 | Ujenzi wa wa viwanja vya michezo midogo midogo -GIZ | 633,982,000 | - | 0% |
| 6 | Uendeshaji wa mashindano ya CHAN | - | 2,734,845,120 | 100% |
| | **JUMLA** | **414,932,196,967** | **195,684,385,669** | **47%** |

**Programu ndogo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Sekta za Vijana, Utamaduni na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 2,437,168,000 | 1,795,159,816 | 74% |
| | **JUMLA** | **2,437,168,000** | **1,795,159,816** | **74%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 315,800,000 | 110,000,000 | 35% |
| | **JUMLA** | **315,800,000** | **110,000,000** | **35%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2025/2026 | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu Pemba | 1,376,614,000 | 990,446,698 | 72% |
| | **JUMLA** | **1,376,614,000** | **990,446,698** | **72%** |

***KIAMBATISHO NAMBA 1E***

***FEDHA ZILIZOKUSANYWA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 KWA KILA PROGRAMUNDOGO***

**Programu ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa habari**

| NO. | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Idara ya Habari Maelezo | 200,000,000 | 13,274,750 | 7% |
| | **JUMLA** | **200,000,000** | **13,274,750** | **7%** |

**Programu ndogo ya Uimarishaji na uendelezaji wa Utamaduni na Sanaa**

| NO. | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu | 360,000,000 | 279,524,000 | 78% |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 50,000,000 | 10,933,500 | 22% |
| | **JUMLA** | **410,000,000** | **290,457,500** | **71%** |

**Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI | FEDHA ILIYOPATIKANA JULAI 2025 HADI MACHI2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu Pemba | 100,000,000 | 14,705,000 | 15% |
| | **JUMLA** | **100,000,000** | **14,705,000** | **15%** |

***KIAMBATISHO NAMBA 1F***

***BAJETI INAYOOMBWA NA WIZARA YA HABARI, SANAA, UTAMADUNI NA MICHEZO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027***

**TAASISI ZISIZOPOKEA RUZUKU**

| No | IDARA | MAELEZO | BAJETI 2026/2027 |
|---|---|---|---|
| 1 | Afisi Kuu Pemba | Mishahara | 1,148,792,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 430,000,000 |
| **JUMLA** | | | **1,578,792,000** |
| 2 | Mipango, Sera na Utafiti | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 338,812,220 |
| **JUMLA** | | | **338,812,220** |
| 3 | Uendeshaji na utumishi | Mishahara | 1,775,188,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 1,209,500,000 |
| **JUMLA** | | | **2,984,688,000** |
| 4 | Habari Maelezo | Mishahara | 641,572,210 |
| | | Matumizi Mengineyo | 470,500,000 |
| **JUMLA** | | | **1,041,572,210** |
| 5 | Idara ya Utamaduni | Mishahara | 2,371,876,570 |
| | | Matumizi Mengineo | 509,958,000 |
| **JUMLA** | | | **2,881,834,570** |
| 7 | Michezo | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 360,000,000 |
| **JUMLA** | | | **360,000,000** |
| **Jumla ya Mishahara** | | | **5,937,428,780** |
| **Jumla ya Matumizi mengine** | | | **3,318,770,220** |
| **Jumla Kuu kwa taasisi zisizopokea Ruzuku** | | | **9,256,199,000** |

**TAASISIZA RUZUKU**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Shirika la Magazeti ya Serikali | Mishahara | 1,260,381,000 |
| | | Matumizi Mengineo | - |
| | | | **1,260,381,000** |
| 2 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | Mishahara | 3,495,180,000 |
| | | Matumizi Mengineo | - |
| | | | **3,495,180,000** |
| 3 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | Mishahara | 2,213,260,000 |
| | | Matumizi Mengineo | - |
| | | | **2,213,260,000** |
| 4 | Tume ya Utangazaji | Mishahara | 749,660,000 |
| | | Matumizi Mengineo | 815,220,000 |
| | | | **1,564,800,000** |
| 5 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 700,340,000 |
| | **JUMLA** | | **700,340,000** |
| 6 | Baraza la Sanaa, na Sensa ya filamu | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 829,250,000 |
| | **JUMLA** | | **829,250,000** |
| 7 | Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar | Mishahara | - |
| | | Matumizi Mengineo | 5,695,810,000 |
| | **JUMLA** | | **5,695,810,000** |
| | | | |
| | **Jumla ya Mishahara Ruzuku** | | **6,968,821,000** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ruzuku** | | **7,225,400,000** |
| | **JUMLA KUU YA RUZUKU** | | **14,194,221,000** |
| | | | |
| | **Jumla ya Mishahara kwa Wizara** | | **13,655,909,780** |
| | **Jumla ya matumizi mengineo ya Wizara** | | **11,359,390,220** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (Matumizi ya kawaida) A** | | **25,015,300,000** |

| | | |
|---|---|---|
| | **MIRADI YA MAENDELEO** | |
| 1 | Mradi wa Mji wa Michezo - Fumba. | 186,872,560,000 |
| 2 | Ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Mikoa | 18,029,760,000 |
| 3 | Mradi wa Ujenz wa Kijiji cha Utamaduni | 15,000,000,000 |
| | **Jumla ya Miradi ya Maendeleo B** | **219,902,320,000** |
| | **JUMLA KUU YA WIZARA (A+B)** | **243,352,740,000** |

***KIAMBATISHO NAMBA 1G***

***BAJETI INAYOOMBWA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KWA KILA PROGRAMU NDOGO***

**Programu Ndogo ya Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa, Ubunifu na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utamaduni | 2,881,834,570 |
| 2 | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu | 829,250,000 |
| 3 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 700,340,000 |
| 4 | Mradi wa Ujenzi wa Kijiji cha Utamaduni | 15,000,000,000 |
| | **JUMLA** | **19,411,425,570** |

**Programu Ndogo ya Uendelezaji wa Miundombinu ya Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Michezo | 360,000,000 |
| 2 | Baraza la Michezo | 5,695,810,000 |
| 3 | Mradi wa Mji wa Michezo - Fumba. | 186,872,560,000 |
| 5 | Ujenzi wa viwanja vya Wilaya na Mikoa | 18,029,760,000 |
| | **JUMLA** | **210,958,130,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Mipango Mikuu ya Wizara**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Mipango Sera na Utafiti | 338,812,220 |
| | **JUMLA** | **338,812,220** |

**Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Wizara ya Habari Sanaa Utamaduni na Michezo**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Idara ya Utumishi na Uendeshaji | 4,902,292,000 |
| | **JUMLA** | **4,902,292,000** |

**Programu Ndogo ya Upatikanaji na Usambazaji wa Habari**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji Zanzibar | 3,495,180,000 |
| 2 | Idara ya Habari Maelezo | 1,041,572,210 |
| 3 | Shirika la Magazeti | 1,260,381,000 |
| | **JUMLA** | **5,797,133,210** |

**Programu Ndogo ya Usimamizi wa vyombo vya Habari, Utangazaji na Uchapaji**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI |
|---|---|---|
| | | |
| 1 | Idara ya Habari Maelezo | 70,500,000 |
| 2 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 2,213,260,000 |
| | **JUMLA** | **2,283,760,000** |

**Programu Ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Ofisi Kuu Pemba | 1,578,792,000 |
| | **JUMLA** | **1,578,792,000** |

***Tume ya Utangazaji Zanzibar***

| NO | Programu | BAJETI 2026/2027 MATUMIZI |
|---|---|---|
| 1 | Maendeleo ya Habari na Utangazaji | 331,155,000 |
| 2 | Utumishi na Uendeshaji | 1,233,725,000 |
| | **Jumla** | **1,564,880,000** |

***KIAMBATISHI NAMBA 1 H***
***MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027***

**MAPATO YANAYOINGIA HAZINA**

| NO. | TAASISI | BAJETI 2026/2027 |
|---|---|---|
| 1 | Baraza la Sanaa na Sensa ya Filamu | 370,000,000 |
| 2 | Baraza la Kiswahili Zanzibar | 41,500,000 |
| 3 | Idara ya Habari Maelezo | 93,500,000 |
| 4 | Baraza la Taifa la Michezo | 6,500,000 |
| 4 | Ofisi Kuu Pemba | 70,000,000 |
| | **JUMLA** | **581,500,000** |

| NO | TAASISI | BAJETI 2026/2027 |
|---|---|---|
| 1 | Shirika la Utangazaji (ZBC) | 3,602,440,000 |
| 2 | Shirika la Magazeti | 1,800,000,000 |
| 3 | ZGP | 8,985,387,000 |
| 4 | Tume ya Utangazaji | 400,000,000 |
| | JUMLA | 14,878,827,000 |

**KIAMBATANISHO NO 11MRADI WA UJENZI WA VIWANJA VYA WILAYA NA MIKOA**

| S/N | MKOA/WILAYA | MAHALI | % YA UTEKELEZAJI |
|---|---|---|---|
| 1 | Mkoa wa Mjini Magharib | Matumbaku | 10 |
| 2 | Mkoa wa Kaskazini Unguja | Pangatupu | 90 |
| 3 | Mkoa wa Kusini Unguja | Kitogani | 100 |
| 4 | Mkoa wa Kaskazini Pemba | Kinyikani | 65 |
| 5 | Mkoa wa Kusini Pemba | Kangani | 99 |
| 6 | Wilaya ya Mjini | Kilimani Brizy | 100 |
| 7 | Wilaya ya Magharibi A | - | 0 |
| 8 | Wilaya ya Magharibi B | Mombasa | 99 |
| 9 | Wilaya ya Kati Unguja | Unguja Ukuu | 99 |
| 10 | Wilaya ya Kusini Unguja | Mwehe-Makunduchi | 99 |
| 11 | Wilaya Kaskazini A | Matemwe- Kijini | 65 |
| 12 | Wilaya ya Kaskazini B | Kitope | 100 |
| 13 | Wilaya ya Wete | Pandani | 85 |
| 14 | Wilaya ya Micheweni | Gongoni-Micheweni | 99 |
| 15 | Wilaya ya Chake | Gombani | 100 |
| 16 | Wilaya ya Mkoani | Ukutini | 95 |
| 17 | Maisara Complex | Maisara | 100 |
| 18 | Mau ze Dong | Mau ze Dong | 100 |

**KIAMBATANISHO NO 1J WAFANYAKAZI WALIOJENGEWA UWEZO KWA KUPATIWA MAFUNZO**

| IDARA | KUWAJENGEA UWEZO WAFANYAKAZI | | | |
|---|---|---|---|---|
| | MUDA MREFU | | MUDA MFUPI | |
| | W'ME | W'KE | W'ME | W'KE |
| OFISI KUU PEMBA | 1 | - | 6 | 4 |
| IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI | 3 | 4 | - | - |
| IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI | 1 | - | - | - |
| IDARA YA MICHEZO | 1 | 3 | - | - |
| IDARA YA HABARI MAELEZO | 1 | 2 | 5 | 6 |
| IDARA YA UTAMADUNI | 1 | 3 | 2 | 5 |
| SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZBC | 2 | 2 | 26 | 31 |
| SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI | 1 | 1 | 33 | 35 |
| WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI | 3 | 4 | 15 | 10 |
| BARAZA LA TAIFA LA MICHEZO | 1 | - | 17 | 7 |
| BARAZA LA KISWAHILI | 1 | - | 9 | 12 |
| BARAZA LA SANAA NA SENSA YA FILAMU | 1 | - | 11 | 16 |
| TUME YA UTANGAZAJI | - | 2 | 13 | 24 |